UKURASA 2

**Gavana** Tutuba awaondoa hofu wananchi usalama mifumo ya fedha



UKURASA 3

**UWT** waonya watendaji kuhusu rushwa

UKURASA 7

**Ufalme**, usultani viongozi upinzani unaua vyama vyao





Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Desemba 22, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581898
www.ippmedia.com
JUMAPILI
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Mount nje ya dimba muda mrefu**

UKURASA 22

# Mbowe rasmi vitani

• **Atangaza** kutetea kiti, atamba hamwogopi Lissu, ajibu tuhuma ufisadi... *Endelea Ukurasa 2*



Mwenyekiti wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo Chadema, Freeman Mbowe, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuhusu msimamo wake wa kugombea nafasi ya Uenyekiti wa chama hicho katika uchaguzi ujao wa kuchagua viongozi mbalimbali wa chama. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

UKURASA WA 5

**NCHEMBA APONGEZA SAUDI ARABIA KWA KUFADHILI MIRADI YA MAENDELEO**

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ameushukuru Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (SFD), kwa mchango wake katika...



**Mwinyi asema kauli zake si porojo kisiasa**

UKURASA 3

**RIPOTI MAALUMU**

## Wataalamu waonya ulaji kuku vifaranga



UKURASA 4

**MICHEZO** TANZANIA YAPANIA UBINGWA WA CHAN UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mbowe rasmi vitani, atangaza kutetea kiti

**Na Restuta James**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, ametangaza rasmi kugombea kiti hicho, huku akijibu hoja za maridhiano, ubadhirifu wa fedha na rushwa.

Aidha, jana alichukua fomu ya kutetea nafasi hiyo ambayo anachuana na Makamu wake, Tundu Lissu, na anatarajia kuirejesha leo.

Mbowe ambaye alihutubia kwa saa 1:18, kwenye mkutano wake na wahariri wa habari pamoja na waandishi wa habari, uliofanyika nyumbani kwake, Mikocheni mkoani Dar es Salaam, alinukuu kauli 10 za viongozi mashuhuri duniani kuhusu maridhiano.

Alisema kinachomsukuma kugombea uongozi kwa awamu nyingine ni dhamira yake ya kuhakikisha CHADEMA inaendelea kuwa chama kikubwa na hatimaye kushika dola.

"Hakuna kiwango cha matusi, kejeli wala dharau kinachoweza kuniondoa Mbowe kuifikiria kesho ninayoitamani. Na kesho ninayoitamani ni kuona chama hiki kikiwa na nguvu na uwezo wa kuongoza serikali ya nchi hii kuleta uhuru wa kweli na maendeleo ya kweli kwa wananchi," alisema.

Alisema watu wanaompinga na kumkejeli hawamnyimi usingizi kwa kuwa anawaza namna ya kujenga CHADEMA imara.

"Nikiangalia minyukano ndani ya mitandao, naona kabisa makundi yanasigana pasipo sababu. Nimeonya mara nyingi na ninaonya tena tusije baadaye tukatafutiana lawama kwenye chama. Baada ya mwezi mmoja, uchaguzi utakuwa umekwisha. Tutakuwa wageni wa nani?

"Nimesema mara nyingi sana nataka kuondoka, lakini siwezi kuondoka katikati ya minyukano iliyopo. Kwa hiyo CHADEMA nipo, nitakuwapo, nitagombea na mimi na viongozi wenzangu wanaoniunga mkono na wasioniunga mkono. Naamini tutakutana kwenye mazungumzo tukiweke chama chetu," alisema na kusisitiza kuwa anayetaka kugombea wakutane kwenye sanduku la kura.

"Tufanye kampeni za kistaarabu. Kila mmoja afanye kampeni akitambua ana wajibu wa kukilinda chama. Wanaoniunga na wasioniunga mkono, watambue naheshimu haki yao lakini hawana haki ya kunitukana," alisisitiza

Alisema kiongozi yeyote atakayeshinda kukiongoza anahitaji watu wote wakiwamo walioshindwa ili kuendelea kukijenga.

"Hii minyukano inahitaji utu uzima. Nimeangalia na nimetafakari kwa kina. Tunahitaji Katiba kwa kucheza miguu yote, ya diplomasia, ushirikishwaji, barabara na kila silaha itumike. Na hii ni ajenda ya msingi katika chama chetu," alisema.

Alisema ajenda nyingine ni mifumo mizuri ya uchaguzi itakayoweka uwazi, uhuru na haki pamoja na sheria nzuri za uchaguzi, ambazo ni miongoni mwa hoja 11 zilizokuwa zimewasilishwa kwenye meza ya maridhiano.

Mahitaji hayo ya Watanzania, alisema yanahitaji mazungumzo na




makundi yote, wakiwamo wanasiasa, taasisi za kidini, wanasheria na wanazuoni. Alisema pamoja na minyukano inayoendelea mitandaoni, chama hicho kiko imara na hakitapasuka wala kufa.

Kuhusu ukomo wa madaraka, alisema unapaswa kufanywa kwenye sanduku la kura na chama hicho kina uhuru wa kidemokrasia kuchagua na kuchaguliwa.

"Sijui ni kigezo gani kinatumika kusema Mbowe amechoka. Sijachoka. Ninaweza kufanya mikutano nane kwa siku bila kula. Namtaka huyo mwenye nguvu hii kuliko mimi. Nimekaa CHADEMA miaka 33 ya shuruba," alisema.

**AJIBU TUHUMA**

Kuhusu tuhuma zinazotolewa na Lissu kwamba kuna baadhi ya viongozi wamekula rushwa, alisema si za kweli na kwamba kama zina ushahidi zinapaswa kuwasilishwa kwenye kamati ya nidhamu inayosiamamiwa na kiongozi huyo (Lissu).

Alisema Lissu ana mamlaka ya kumwamuru Katibu Mkuu wa chama kumwandalia kikao na kwamba madai kuwa ofisi hiyo haijatekeleza hilo si ya kweli.

Mbowe alianza kwa kunukuu kauli 10 za viongozi mashuhuri duniani, akiwamo Hayati Nelson Mandela aliyekuwa mpigania uhuru na Rais wa Afrika Kusini, Makatibu Wakuu wastaafu wa Umoja wa Mataifa, Ban Ki-Moon na Koffi Anan, marais wa Marekani, Jonh Kennedy na Barack Obama, Kansela mstaafu wa Ujerumani, Angela Markel, Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza, Wiston Churchil na Waziri Mkuu wa India, Mahatma Gandhi, ambao kwa nyakati mbalimbali walihimiza umuhimu wa maridhiano hasa kunapotokea tofauti kubwa za kisiasa.

Alisema Kamati Kuu na Baraza Kuu la CHADEMA, waliomba mara kadhaa kufanya mazungumzo na Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli, ili kutafuta mkwamo wa kisiasa wakati huo lakini alikataa na kwamba Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani, alikubali ombi hilo.

Alisema anaamini kwamba hata sasa, chama hicho kimefanikiwa kufanya uchaguzi katika ngazi mbalimbali kutokana na maridhiano ambayo yalifanikisha kufuta katazo la miaka saba la kuzuia mikutano ya vyama vya siasa.

"Maridhiano si jambo jepesi lakini ni jambo lisiloepukika katika siasa duniani kote. Makundi mbalimbali yanachukua upande wa maridhiano kutokana kile inachotamani," alisema.

Alisema CHADEMA ilikuwa na hoja 11 kwenye mazungumzo hayo kati yake na serikali pamoja na Chama Cha Mapinduzi (CCM) zilizofanikisha zaidi ya kesi 400, zilizokuwa zimebambikwa kwa makada na viongozi wake kufutwa, wafungwa wa kisiasa kuachiwa huru, kufunguliwa kwa mikutano ya kisiasa na kulipwa ruzuku ambayo ni stahiki ya chama hicho.

Hata hivyo, alisema maridhiano yalipingwa na wahafidhina pamoja na wanufaika wa uchaguzi mbovu wa mwaka 2020, ndani ya CCM. Alisema upinzani wa maridhiano ndani ya CCM uliongezewa nguvu na ule uliokuwa ndani ya CHADEMA.

"Mtu yeyote unayejaribu kutaka akuunge mkono, anatarajia kuona unamheshimu na mkubali kukosa ili kupata kikubwa zaidi mnachokitaka wote. "Ninajivunia sana mazungumzo na uamuzi wetu wa kuingia kwenye maridhiano," alisema.

Katazo la mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa, alisema liliiumiza zaidi CHADEMA kwa kuwa wabunge, madiwani na viongozi wake wa ngazi mbalimbali waliumizwa na wengine kuuawa, jambo lililowafanya wananchi waogope kuwa upande wa vyama vya upinzani.

Alisema pamoja na kwamba maridhiano yalikwama, Tanzania inahitaji Katiba Mpya, Mifumo huru ya uchaguzi na sheria nzuri za kusimamia uchaguzi. Alisema chama hicho kimeazimia kutengeneza ajenda za kitaifa ambazo ni Katiba Mpya, mifumo huru ya uchaguzi na sheria nzuri, ambazo hakiwezi kusimama peke yake na kufanikiwa kuzipata.

**TUHUMA RUSHWA**

Alisema hawezi kuiuza CHADEMA kwa ahadi ya cheo kikubwa serikalini; na kwamba angetaka kufanya hivyo angekubali ahadi za hayati Magufuli.

"Aliniahidi ahadi zote duniani. Aliniambia nijiunge na CCM nichague cheo chochote unachotaka, nikamwambia sitaki. Akasema achana na CHADEMA chagua biashara yoyote unayotaka nitakurejeshea mali zako zote ulizonyang'anywa, nikakataa. Siwezi kukubali sasa hivi," alisema na kuongeza kuwa hajaahidiwa cheo wala fedha kutoka sehemu yoyote.

Kuhusu ubadhirifu, alisema CHADEMA inaendeshwa kwa michango ya wanachama na kwamba kwa miaka mitano mfululizo, imepata hati safi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

## Gavana awatoa hofu wananchi usalama wa mifumo ya kifedha

**Na Getrude Mbago**

GAVANA wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba, amewahakikishia Watanzania kuwa mifumo yote ya malipo inayohusisha akaunti za serikali, benki na simu za mkononi iko salama na madhubuti.

Kutokama na hali hiyo, amesema mifumo hiyo inawezesha kufanyika miamala kiurahisi na usalama.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi wakati wa ziara ya baadhi ya viongozi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kushukuru mchango wa benki hiyo katika ulipaji kodi, Gavana Tutuba aliwataka wananchi kuhakikisha wanatumia mifumo rasmi ya malipo ili kuhakikisha fedha zao zinaingia salama katika akaunti zinazohusika.

"Mifumo yetu iko imara na inafanya kazi bila changamoto. Ukilipa kwa hundi, akaunti ya benki au kutoka akaunti kwenda kwa simu, kila njia iko salama. Akaunti zote za serikali ziko salama na fedha zinaingia moja kwa moja bila vikwazo vyovyote," alisema Tutuba.

Pia alisema BoT inasimamia akaunti zote za serikali pamoja na benki na pia inahakikisha usalama wa fedha zilizohifadhiwa kwenye kampuni za simu.

Kwa mujibu wa Tutuba, timu za kitaalamu za ufuatiliaji wa uhalifu mtandaoni zinafanya kazi saa 24 kuhakikisha hakuna vitisho vya usalama vinavyoathiri mifumo hiyo.

"Kazi yetu ni kuhakikisha kuwa mifumo inafanya kazi muda wote na hata wale wanaojaribu kudukua wanashindwa kwa sababu tunadhibiti kila kitu kwa wakati," alisisitiza.

Mkurugenzi wa Fedha wa TRA, Dinah Edward, alisema mamlaka hiyo inatarajia kukusanya kodi ya Sh. trilioni 15.27 kuanzia Januari hadi Juni, mwakani huku Desemba, mwaka huu, ikiwa na lengo la kukusanya Sh. trilioni 3.46.

Edward alisema lengo hilo ni sehemu ya mpango wa kufanikisha ukusanyaji wa Sh. trilioni 31.05 kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Mpaka kufikia Novemba, mwaka huu, TRA imekusanya Sh. trilioni 12.94 sawa na asilimia 105.1 ya malengo ya kipindi hicho au asilimia 41.67 ya lengo la mwaka mzima.

"Tunatarajia kuweka rekodi mpya ya ukusanyaji kodi lakini mafanikio haya yanahitaji ushirikiano mzuri kati yetu, walipakodi na wadau mbalimbali," alisema.

Edward alibainisha kuwa TRA imeweka mikakati ya kuboresha mazingira ya ukusanyaji kodi kwa kuimarisha mifumo ya kielektroniki na kushirikiana na taasisi mbalimbali, ikiwemo BoT, ili kuhakikisha malengo yanafikiwa.

**USHIRIKIANO BOT, TRA**

Gavana Tutuba alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya BoT na TRA kwa lengo la kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato. "Tunashirikiana kikamilifu kuhakikisha kila malipo yanafanyika kwa njia salama na rahisi," alisema.

Aidha, aliipongeza TRA kwa kufanikisha ukusanyaji wa mapato kwa asilimia 105 kwa kipindi cha miezi sita iliyopita, hatua aliyosema ni ishara ya jitihada madhubuti za mamlaka hiyo.

HABARI KITAIFA

# UWT waonya watendaji kuhusu kutoa rushwa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MWENYEKITI wa Taifa wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mary Chatanda, amekemea tabia za baadhi ya makatibu wa mikoa na wilaya wa jumuiya hiyo kutoa zawadi za Sh.10,000, kanga na vitenge kwa wajumbe wa umoja huo kwa malengo yao binafsi.

Amesema tabia hiyo ni kinyume cha taratibu za chama na hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa yeyote atakayebainika kufanya hivyo.

Chatanda aliyasema hayo jana kwenye hafla ya ugawaji wa misaada iliyoandaliwa na Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Ruvuma, Jacklin Msongozi, katika ukumbi wa mikutano wa Familia Takatifu, Bombambili, Manispaa ya Songea.

Misaada iliyotolewa ni mashine 20 za kukamulia alizeti, vyerahani 700, majiko banifu 300 ya gesi, mifuko ya simenti 100, mikeka ya nyumba za ibada misikiti minne na ng'ombe wawili wa maziwa kwa familia mbili zenye kipato duni.

Alisema kuna baadhi ya viongozi wasio waaminifu wenye nia ya kugombea nafasi mbalimbali wanaotengeneza mianya ya rushwa kwa wajumbe kwa kuwapa pesa na vitenge.

Chatanda alisema UWT kwa kushirikiana na kamati za maadili, haitawafumbia macho watu hao na kusisitiza kuwa hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

Alisema viongozi wa UWT wanapaswa kutoa huduma kwa jamii kwa kujali na si kwa manufaa binafsi na kuhimiza uwazi na maadili bora katika uongozi na si vinginevyo.

"Twendeni tukawatumikie wanawake wana changamoto chungu nzima. Twendeni tukawatembelee wanawake tuzungumze nao, tutafute fursa kama hizi ambazo amefanya Mbunge Msongozi tuwapelekee. Ukimwezesha mwanamke umeliwezesha taifa zima.

"Lakini na wao nawaambia kwamba marufuku kuwafuata wale wanaowapigia kura na hii nawaambia ukweli hatuwatendei haki wanawake wale ambao waliwachagua kwa kuwapa Sh.10,000, "alisema Chatanda.

Alisema Chama Cha Mapinduzi (CCM) kinawategemea sana wanawake walioko kwenye vijiji kwa kuwa ndio wanaokiwezesha kushinda, hivyo ni lazima wawatembelee, wazungumze nao ili wajue changamoto zao na kuzifanyia utatuzi kama alivyofanya Msongozi.

Chatanda alimpongeza Msongozi kwa kuwa miongoni mwa wabunge wachache wanawake ambao wanafanya vizuri kwa kuwainua wanawake na makundi mengine.

Msongozi alisema wamegawa vifaa hivyo ili kuwezesha vikundi vya wanawake na vijana wa mkoa huo kujikwamua kiuchumi ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan.

Tukio hilo liliambatana na utoaji wa taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 -2025 katika sekta za kilimo, ufugaji, viwanda, nishati, elimu na lishe.

Alisema uhitaji wa mafuta nchini ni mkubwa wakati uzalishaji ni mdogo, akibainisha kuwa uzalishaji huo kwa sasa nchini ni tani 290,000 sawa na asilimia 45 ya mahitaji ya mafuta ya kula ambayo ni tani 650,000 kwa mwaka.

Ofisa Biashara wa Mkoa wa Ruvuma, Joseph Martin, alisema kwa kushirikiana na mbunge huyo, ofisi yake itatoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wanavikundi wote juu ya utunzaji wa kumbukumbu za hesabu, ufungashaji, umuhimu wa usajili wa biashara, taratibu za uendeshaji wa biashara kwa kufuata sheria za kibiashara, kujitangaza kibiashara na mambo mengine.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Rundo la takataka likiwa limetelekezwa katika kituo cha bajaji Kitunda jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwinyi asema kauli zake si porojo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema mambo yote anayoyatamka hadharani kuhusu utekelezaji wa miradi mikubwa zaidi ya maendeleo, si porojo za kisiasa bali ni dhamira yake ya kweli ya kufikia azma hiyo.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Mawasiliano Ikulu, Zanzibar, ilisema Rais Mwinyi alitoa kauli hiyo alipofungua maonesho ya kwanza ya ghorofa Malindi Zanzibar, Shehia ya Mchangani, wilaya ya Mjini Mkoa wa Mjini Magharibi ikiwa ni shamrashamra za miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Dk. Mwinyi alisema kufanya hivyo ni kuonesha uongozi unaoacha alama na uzalendo pamoja na kuwahakikishia wananchi kwa kaulimbiu inayosema "Yajayo ni Makubwa Zaidi."

Aliitaja miradi mingine mikubwa ya kimkakati inayotarajiwa kutekelezwa miaka ijayo chini ya uongozi wake kuwa ni pamoja na mradi wa teksi za baharini ambapo ujenzi wa bandari za teksi hizo umeanza Maruhudi.

Alisema teksi hizo zitapakia na kushusha abiria watakaotumia usafiri wa maji kuelekea maeneo ya mkoa wa Kaskazini Unguja badala ya usafiri wa nchi kavu wa daladala na usafiri mwingine.

Miradi mingine, kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, ni wa treni zitakazotumia barabara za lami kutoka Malindi mjini hadi Bububu, ujenzi wa barabara nne za juu zenye mapishano.

Dk. Mwinyi pia aliwatoa hofu wananchi wa Mji Mkongwe kwamba serikali inatekeleza miradi yake huku ikiwa na dhamira njema ya kuuendeleza urithi wa kimataifa kwa lengo la kuulinda mji huo na si kuuharibu.

Alisema uzinduzi wa maegesho ya magari Malindi una nia ya kupunguza msongamano wa magari makubwa na madogo yanayoingia na kutoka Mji Mkongwe.

Dk. Mwinyi pia alibainisha kuwa mbali na maegesho hayo, nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kujenga kituo cha kisasa cha mabasi ya abiria pembezoni mwa maegesho ya gari Malindi, sambamba na ujenzi wa kituo kikubwa cha magari ya abiria na kiwanja cha michezo kwa vijana.

Alisema kupitia mradi wa "Big Z", serikali pia inakusudia kujenga mradi wa barabara ya kisasa kutoka Malindi hadi hospitali ya Mnazi Mmoja ikiwa ni hatua ya kuupandisha hadhi Mji Mkongwe pamoja na kuwa na mradi wa kuweka nyaya zote za umeme, maji na mawasiliano chini ya ardhi ili kuimarisha usafi wa mji huo kwa kuikarabati upya kwa kuiboreshea haiba njema "Jamhuri Garden" ili iwe na mwonekano wa kisasa.

Aidha, Rais Mwinyi ameupongeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kwa kutoa mafao kwa wananchi kwa wakati na kwa kiwango kizuri, kuwekeza kwenye miradi yenye tija na kufanikiwa kutoa mchango kwa maendeleo ya nchi kwa kujenga miradi mikubwa. Akitolea mfano mataifa mengine duniani, alisema mifuko ya hifadhi ya jamii ndiyo inayojenga nchi, hivyo aliitaka ZSSF kuendeleza utaratibu huo.

Dk. Mwinyi pia aliwasisitiza wanachi kuendelea kuidumisha amani ya nchi, umoja na mshikamano ili nchi iendelee kupiga hatua kubwa za maendeleo.

Amempongeza mkandarasi Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) na Mshauri Elekezi kwa CCEC kwa kufanikisha ujenzi wa maegesho ya magari Malindi kwa viwango cha hali ya juu na kuzingatia wakati.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mita na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohammed, ambaye pia amemwakilisha Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema maendeleo anayoyafanya Rais Dk. Mwinyi, yamewafilisi watu wasioitakia mema Zanzibar.

Pia alisema wananchi watamkumbuka kwa kuacha alama ya uongozi wake na kuonesha uzalendo alionao kwa nchi.

Kuhusu gharama za ujenzi wa maegesho hayo, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Juma Malik Akili, alisema Sh. bilioni 6.8 zilitumika na kuwasisitiza wananchi kuendelea kuwasilisha michango yao ZSSF ili miradi mikubwa zaidi ya maendeleo iendelee kutekelezwa na mfuko huo.

Katibu Mkuu alisema maegesho hayo yana uwezo wa kuchukua magari 200 hadi 220 kwa wakati mmoja.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

Nipashe
WhatsApp Chaneli
Skani hapa kutembelea chaneli yetu

RIPOTI MAALUM

# Hatari ulaji kuku vifaranga

## -Wataalam wasema huchangia usugu wa dawa mwilini

Na Jenifer Gilla



KUKU wa kisasa ni moja ya vitoweo vinavyopendwa katika maeneo mbalimbali nchini. Katika sehemu mbalimbali, watu wamekuwa wakitumia kitoweo hicho kikiwa kimechomwa au kukaangwa sambamba na vyakula vingine kama ugali na chipsi. Matumizi makubwa yamekuwa katika vibanda vya chipsi au migahawa.

Pamoja na umaarufu na kupendwa na watu wengi, wataalamu wanaonya endapo wafugaji hawatazingatia taratibu za ufugaji, kuna madhara makubwa ambayo yatampata mtumiaji, ikiwamo kutengeneza usugu wa dawa kwa binadamu.

Wanasema kuku huwa tayari kwa matumizi wanapofikisha umri wa kuanzia mwezi mmoja na kuendelea lakini kwa sasa baadhi ya wafugaji huwaingiza sokoni wakiwa na umri wa chini ya wiki tatu tangu walipoanguliwa vifaranga.

Uchunguzi wa Nipashe katika masoko mbalimbali mkoani Dar es Salaam yakiwamo ya Shekilango na Mwananyamala, umebaini asilimia kubwa ya kuku wa kisasa hupokewa tayari kwa kuuzwa wakiwa bado ni vifaranga ambao hawajatimiza mwezi, kama wataalam wa mifugo wanavyoshauri.

Nje ya masoko hayo, wahitaji wengi wa kuku ni pamoja na mama lishe na wakaanga chipsi, ambao asilimia kubwa ya watu huwategemea katika mlo mmojawapo wa siku.

Amina Said, mama lishe aliyekutwa katika soko la Shekilango akinunua kuku, anakiri hali ya kuku wanaoingizwa sokoni hivi sasa hawastahili kwa ulaji kwa sababu ni wadogo, wanapowanyonyoa huwa kama ndege.

"Wateja wetu wanalalamika wanaona kama tunawauzia kuku wadogo, lakini bei ya chakula haijabadilika ipo palepale. Ushauri wetu wafugaji wahakikishe kuku wanayemleta sokoni angalau basi awe na miezi miwili na kuendelea," alishauri.

Anthony Lyimo, mkaanga chipsi ambaye alikutwa soko la Mwananyamala akinunua mahitaji yake, wakiwamo kuku, alishauri wizara husika (ya Mifugo na Uvuvi), kutoa elimu kwa wafugaji ili kuepuka kupeleka sokoni kuku wakiwa vifaranga.

"Tunachouziwa sokoni ni vifaranga, vingine havieleweki. Unajiuliza ni wazima kweli? Halafu kwa umri chini ya mwezi wanakuwa kwenye hatua ya kukuzwa na dawa mbalimbali. Hatujui ulaji wa kuku wa aina hii athari zake kwa binadamu ni zipi. Chipsi kuku ni Sh. 3,500 na kwingine 4,500. Wateja wanalalamika kuwa kuku ni wadogo," anasema.

Hamisi Ramadhani, mfanyabiashara wa kuku katika soko la Shekilango, anasema wanalazimika kuwachukua kuku hao kabla ya muda unaotakiwa kuingizwa sokoni kwa sababu upatikanaji wake kwa sasa ni wa shida. Anasema kuna wakati wanakosa hata kuku mmoja wa kuuza huku uhitaji sokoni ukiwa mkubwa,

"Wafugaji wanatupigia simu wanauza kuku wakiwa na wiki tatu. Kutokana na uhitaji sokoni, tunalazimika kuwachukua ili wakulie hapo sokoni lakini wateja wakija wanawataka vivyo hivyo.

"Ninauza kuku lakini ninanunua huko shamba la Bagamoyo kwa wafugaji. Kwa mfano leo (juzi) kuku wameadimika sana. Ukienda shambani ukiacha kuchukua kwa kuwa hawajatimiza muda, unakuta mwingine kachukua," anasema.

Mfanyabiashara mwingine, Juma Mlupili, anasema kinachosababisha kuadimika kwa kuku na kufanya kuuzwa kabla ya muda ni kupanda kwa bei za vyakula. Anasema kuku hao wanapofika wiki tatu wafugaji huwapigia simu na kuwauza kwa sababu wanakimbia gharama za ufugaji wanazodai kwa sasa ni kubwa.

"Inawezekana sababu ikawa kupanda kwa bei za vyakula, wafugaji wanauza mapema ili wapate faida wasiendelee kuwalisha mpaka watimize muda wa kitaalamu,"anasema.

Mlupili anataja sababu nyingine kuwa ni msimu huu wa sikukuu mahitaji ya kuku hayo yanaongezeka kwa kuwa wafugaji wengi hasa wachaga wanakwenda kula sikukuu mkoani. "Inawezekana pia wafanyabiashara wamehifadhi kuku ndani waje kuwauza siku ya sikukuu, maana wengi wanavizia siku hiyo wakijua kuwa bei itakuwa juu wapate faida zaidi," anasema.

### KAULI YA WAFUGAJI

Mfugaji wa Kuku kutoka Mapinga, Bagamoyo mkoani Pwani, Musa Jackson, anasema kinachosababisha wauze kuku kabla ya muda ni gharama kubwa za chakula cha kuku. Anasema watu wengi wanaacha kujihusisha na biashara hiyo wameona hawapati faida kutokana kuongezeka kwa gharama za dawa na chakula cha kuku.

"Kwa mfano pumba ya kuku mwaka juzi gunia lilikuwa Sh. 20,000 sasa hivi ni Sh. 32,000 na ukiangalia hakuna dalili za kushuka kwa hizo gharama. Hata gharama za dawa za kutibu kuku na za madaktari wanaopima kuku nazo zimepanda na kusababisha uendeshaji kuwa juu.

"Serikali iweke bei elekezi kwa vyakula vya kuku ili kusaidia wafugaji wapate vyakula kwa bei inayofanania maana maduka mengine yanauza kwa gharama kubwa sana hali inayokatisha tamaa," anasema.

Mfugaji mwingine kutoka Kivule, Dar es Salaam, Msafiri Ngonyani, anaungana na Jackson akisema gharama za vyakula vya kuku kuwa juu ndiyo sababu ya wao kuuza kuku wakiwa chini ya muda.

"Kuku anapokaa kwa muda mrefu anatumia chakula kingi na gharama kubwa. Ukija kupiga hesabu ukimuuza kwa Sh. 5,500 hupati faida. Kwa hiyo kinachotokea mfugaji anatangaza anauza kuku hata kama hawajafikisha muda ili asiendelee kupata gharama," anasema.

Ngonyani anasema baadhi ya mbegu za kuku hao wa kisasa mbegu zao zimedumaa hata akifika wiki nne bado ataonekana mdogo.

### MADHARA MWILINI

Mganga wa mifugo, Dk. Allen Audax, anasema kwa ufugaji wa Kitanzania, kuku wanakuwa tayari kwa matumizi wanapofikisha umri kuanzia mwezi mmoja na kuendelea.

Anasema kuku aliye chini ya wiki nne, wakati mwingine anakuwa bado anatumia dawa, hivyo akiuzwa na mtu akala maana yake atakuwa anakula dawa iliyokuwa ndani ya kuku huyo.

Pia anasema katika kila dawa anayopewa kuku, kuna maelekezo ya kuwa anaweza kuliwa kwa muda fulani baada ya kupewa dawa hiyo na kwamba akiliwa kabla ya muda wa maelekezo kwisha, mlaji anakuwa amekula na dawa iliyo ndani ya kuku.

"Kwa hiyo kama mtu akiwa ana tabia ya kula kuku ambao bado dawa hazijaisha ndani ya miili yao, ina maana dawa za kuku zitakuwa zinaingia mwilini mwake. Matokeo yake mwili wake utakuwa unatengeneza mazoea ya dawa, hivyo siku akija kuumwa na kutumia dawa za binadamu zinaweza zisifanye kazi," anasema.

Dk. Audax alibainisha kuwa kuku wakiwa hawajakomaa wanakuwa na upungufu wa protini na mafuta kulinganisha na kuku waliofikia umri wa kuuzwa, hivyo mtu akila anakosa virutubisho muhimu.

Pia anasema pia kuku hao wakiwa chini ya umri wa kuuzwa wana upungufu mkubwa wa ladha kwa sababu ya upungufu wa protini na mafuta kwenye nyama zao.

Daktari Bingwa wa Tiba ya Familia kutoka Hospitali ya Aga Khan, Willbroad Kyejo, akizungumza kitaalam madhara ya usugu wa dawa kwenye mwili wa binadamu, aanasema kunakuwa na ugumu wa kutibu magonjwa kwa sababu dawa atakazokuwa anatumia mgonjwa haziwezi tena kuua bakteria wanaosababisha ugonjwa.

"Kwa mfano, mtu akipata homa ya mapafu, dawa za kawaida zinaweza kushindwa kufanya kazi na mgonjwa anaweza kuendelea kuwa mgonjwa au hata kufariki dunia," anasema.

Dk. Kyejo alisema pia gharama za matibabu zinaongezeka kwa sababu mwili ukiwa sugu kwa dawa za kawaida, mgonjwa atahitaji dawa za gharama kubwa zaidi au matibabu ya muda mrefu jambo linaloongeza mzigo wa kifedha kwa familia na taifa.

"Madhara mengine ya usugu wa dawa ni mgonjwa kupoteza maisha kwa sababu magonjwa sugu hayawezi kutibika kwa urahisi. Wagonjwa wengi zaidi wanaweza kupoteza maisha, hata kwa maambukizi ya kawaida," anasema.

Pia anasema husababisha maambukizi kuenea kwa urahisi kwa mtu mmoja hadi mwingine, hasa katika maeneo yenye watu wengi kama hospitalini, shuleni au nyumbani.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Nchemba apongeza Saudi Arabia kufadhili miradi ya maendeleo

**Na Benny Mwaipaja,**
SAUDI ARABIA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ameushukuru Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (SFD), kwa mchango wake katika maendeleo ya Tanzania kupitia ufadhili wa miradi mbalimbali ya maendeleo hususan sekta za maji, afya, nishati na ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Dk. Nchemba alitoa shukrani hizo juzi alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa SDF, Sultan Al-Mashard, Kando ya Mkutano wa Jukwaa la Biashara na Uwekezaji, lililofanyika mjini Riyadh, Saudi Arabia.

Dk. Nchemba aliyeambatana na mawaziri wenzake wawili katika kikao hicho, Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema ushirikiano wa Saudi Arabia na Tanzania uliodumu kwa zaidi ya miaka 40 sasa, umekuwa wa mfano.

Aliitaja baadhi ya miradi iliyoleta mageuzi makubwa katika jamii ya Tanzania kuwa ni pamoja na ukarabati wa mradi wa maji mkoani Mara uliogharimu Dola la Marekani milioni 15, ujenzi wa mradi wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe uliogharimu Dola za Marekani milioni 25 na na ujenzi wa barabara za vijijini awamu ya pili Zanzibar wenye thamani ya Dola milioni nne.

Miradi mingine kwa mujibu wa Waziri Nchemba ni ukarabati na upanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja-Zanzibar uliogharimu Dola milioni 15 na kushirikiana na wadau wengine kufadhili mradi wa ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa Kilovolti 220 kuanzia Benako hadi Kyaka wa thamani ya Dola milioni 105.4.

Katika mazungumzo hayo, Dk. Nchemba aligusia utekelezaji wa miradi mingine mikubwa ya kimkakati inayoendelea nchini Tanzania ukiwamo wa reli ya kisasa (SGR), ambao alisema utakapokamilika utakuwa kichocheo kikubwa cha biashara na uchumi katika nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo na Dk. Mkuya, walisema ushiriki wa SDF katika ujenzi wa miradi ya kiuchumi na kijamii nchini Tanzania utachochea maendeleo ya nchi.

Al-Marshad alisema mfuko huo uko tayari kuendelea kuisaidia Tanzania kutokana na uhusiano imara uliopo kwa faida ya wananchi wa nchi hizo mbili.

Alipongeza hatua kubwa zinazochukuliwa na serikali katika kutekeleza miradi muhimu kwa maendeleo ya nchi akiitaja reli ya kisasa inayojengwa kwamba itachochea na kukuza biashara na usafirishaji wa abiria na mizigo katika eneo la mradi.

Katika kikao hicho Tanzania na SDF zilikubaliana kuunda timu ya wataalam watakaopitia, kuchambua na kuchakata miradi mbalimbali ambayo mfuko huo utatoa fedha ili kuimarisha zaidi ushirikiano kati ya Tanzania na Saudi Arabia.



Mchuuzi wa mabegi akitafuta wateja katika eneo la Kitunda jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Polisi yaonya uhalifu Krismasi, mwaka mpya

**Na Jenifer Gilla**

JESHI la Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, limewaonya baadhi ya wananchi wanaotekeleza vitendo vya uhalifu katika kipindi cha sikukuu za Krismas na Mwaka Mpya huku likisisitiza kuwa hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alitaja vitendo hivyo kuwa ni kuendesha vyombo vya moto bila kuzingatia sheria za usalama barabarani na kutumia vilevi wakiwa wanaendesha vyombo hivyo.

Alitaja kundi lingine kuwa ni wenye tabia ya kupiga baruti au fataki bila vibali vya kisheria na katika maeneo ambayo hayaruhusiwi na kuwa polisi hawatasita kuwachukulia hatua watu hao.

"Polisi hawatasita kuchuka hatua kwa mtu yeyote atakaye kiuka sheria za nchi kwa kisingizio cha kufanya mambo ya ovyo chini ya mwavuli wa Krismasi na Mwaka Mpya. Jeshi linawatakia maandalizi mema na kusherehekea kwa amani," alisema

Alisema katika kueleka sherehe za mwisho wa mwaka za Krismasi na Mwaka Mpya, hali ya usalama mkoani Dar es Salaam imeimarika na vikosi vyote vya Jeshi la Polisi Kanda hiyo viko tayari kuzuia vitendo vya kihalifu maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

Kamanda Muliro alisema jeshi hilo pia litaimarisha ulinzi kwenye nyumba za ibada ili kutoa fursa kwa wananchi kushiriki katika ibada zilizoandaliwa kwa ajili ya sikukuu hizo katika hali ya utulivu na amani.

# Majaliwa asisitiza elimu hitaji muhimu kwa Watanzania

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema suala la elimu ni hitaji la muhimu kwa watoto wa Kitanzania na kwamba ujenzi wa shule chini ya mradi wa kuboresha elimu ya sekondari (SEQUIP) ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Majaliwa alisema hayo jana alipokagua ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana ya Mkoa wa Mwanza (Mwanza Girls) na kuweka jiwe la msingi la shule hiyo iliyoko katika kijiji cha Ihushi, kata ya Bujashi, wilayani Magu.

Shule hiyo ni miongoni mwa shule za sekondari za bweni 26 zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 ambazo zinaendelea kujengwa nchi nzima kwa ajili ya wasichana wanaosoma masomo ya sayansi kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita.

Akizungumza na wananchi waliofika shuleni hapo: "Mheshimiwa Rais alielekeza tutekeleze miradi inayogusa moja kwa moja hali ya kila siku ya wananchi. Shule ni hii inakaribia kukamilika.

"Katika Sekta ya Afya. zililetwa Sh. milioni 250 kwa ajili ya zahanati tano, hospitali ya wilaya tayari imekamilika na hivi karibuni, Sh. milioni 700 zililetwa kukamilisha majengo ikiwamo wodi ya wanaume."

Majaliwa alisema kwenye umeme, vijiji 81 kati ya 82 vya wilaya hii tayari vimepata umeme na kijiji kimoja kilichobakia kiko kwenye kisiwa ndani ya Ziwa Victoria lakini tayari mikataba imesainiwa ili maeneo ya visiwani yaweze kupelekewa umeme.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Zainab Katimba, alisema ujenzi wa shule hiyo ambayo iko kwenye hatua za umaliziaji, umegharimu Sh. bilioni 4.5 na kwamba hadi sasa wanafunzi 514 wamekwishaanza masomo kwenye shule hiyo.

Alisema ifikapo Januari, mwakani shule hiyo inatarajiwa kupokea wanafunzi 120 wa kidato cha kwanza.

Awali, Waziri Mkuu alikagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa tangi la kuhifadhi maji la Kisesa, Magu mkoani Mwanza ikiwa ni mpango wa muda wa kati wa kuboresha huduma ya maji jijini Mwanza ambao unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 3.54.

Ujenzi wa tangi hilo lenye ujazo wa lita milioni tano, unafadhiliwa na serikali ya Tanzania pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD).

Hadi sasa, ujenzi wake umefikia asilimia 93 na unatarajiwa kuhudumia wakazi 75,000 wa maeneo ya Kisesa, Bujora, Igudija na maeneo ya jirani pindi utakapokamilika.

Akizungumza na wananchi wa eneo la Kisesa baada ya kukagua mradi huo, Waziri Mkuu Majaliwa alisema serikali imefanya kazi kubwa ya utekelezaji wa miradi mikubwa inayowagusa wananchi moja kwa moja kwenye sekta za elimu, afya, maji, kilimo, uvuvi na barabara.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema wizara hiyo itaendelea kusimamia maagizo ya Rais Samia ya kuhakikisha wananchi wanapata maji katika maeneo yao. "Mheshimiwa Rais Samia alisema hataki kuona wanawake wa nchi hii wakiteseka kutafuta maji," alisema. Alitumia fursa hiyo kumpongeza Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Neli Msuya, kwa kazi kubwa ya kusimamia ujenzi wa miradi ya maji ambayo ilisaidia kuongeza upatikanaji wa maji jijini Mwanza hata kabla ujenzi wa tenki hilo kubwa haujakamilika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jamii itafakari na kuchukua hatua ongezeko mauaji, ukatili

**KWA** muda mrefu sasa kumekuwa na taarifa za kuwapo kwa mauaji kwenye mikoa mbalimbali sambamba na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto. Baadhi ya sababu zinazotajwa kuwa chanzo cha vitendo hivyo ni wivu wa kimapenzi, tofauti kati ya wanandoa na tamaa ya kupata utajiri.

Sababu nyingine inayotajwa ni imani za kishirikina hasa zinazochangia mauaji ya wazee na vikongwe kwamba wanahusika na vifo vya wanafamilia. Katika baadhi ya makabila, imekuwa kawaida kuwa kikongwe au mzee anapokuwa na macho mekundu, anadaiwa kuwa ni mchawi, hivyo hana budi kuuawa kwa kuwa kuendelea kuishi kwake anaweza kusababisha vifo vya watoto na vijana katika eneo husika.

Vitendo hivyo, kwa ujumla, vimekuwa vikishamiri siku hadi siku huku vyombo vya habari vikitangaza matukio hayo yanayotokea kila kona ya nchi. Kutokana na kukithiri huko, wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa serikalli, wa dini na wanaharakati, wamekuwa wakikemea huku wakitaka hatua zaidi zichukuliwe dhidi ya watu watakaobainika kujihusisha na mauaji hayo pamoja na ukatili.

Hali hiyo imesababisha viongozi wa dini hasa maaskofu wakati wa sikukuu kama vile Krismasi, Pasaka, Maulidi na Iddi pamoja na makongamano mbalimbali, wamekuwa wakipaza sauti kutaka hatua zichukuliwe kwa kuwa matukio hayo yanaharibu taswira njema ya taifa iliyojengeka kwa miaka mingi.

Aidha kila mwaka kumekuwa na siku 16 za kupinga ukatili, ikiwa ni sehemu ya kutoa elimu kuhusu madhara ya ukatili na mauaji ya watu wasio na hatia kama vile vikongwe, wanawake na watoto. Pamoja na jitihada zote hizo, bado vitendo hivyo vinaendelea kushamiri na kuota mizizi ndani ya jamii.

Hatua hiyo pia imemwibua Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, ambaye juzi alikuja juu na kuhoji kukithiri kwa matukio ya mauaji, ukatili dhidi ya wanawake na watoto mkoani humo kama yanatokana na matatizo ya afya ya akili au ushetani.

Mtaka alitoa kauli hiyo kwenye kikao na makundi mbalimbali kichofanyika mjini Njombe kujadili jinsi ya kukabiliana na matukio hayo katika jamii, baada ya kuelezwa takwimu za matukio hayo na kuweka bayana kwamba yanachafua sura ya mkoa ambao umekuwa maarufu kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.


Bila kuuma maneno, Mtaka alisema matukio hayo pia yanaondoa ubinadamu na kufedhehesha utu wa mtu na haki katika jamii, hivyo hayavumiliki na hayapaswi kuendelea kutokea ndani ya mkoa huo. Alisema kutokana na kuenea kwa vitendo hivyo, jamii inapaswa kujiuliza chanzo chake ni nini na utamaduni huo unatoka wapi na ni jamii gani inayokusudiwa kujengwa kwa mustakabali wa taifa siku zijazo.

Mkuu huyo wa mkoa alikiri wazi kwamba kwa mtazamo wake, anadhani serikali haijafanya juhudi za kutosha katika suala hilo, hivyo kuna haja ya kufanya mambo makubwa zaidi kukomesha. Pia alishauri jamii na kila mmoja kwenye nafasi yake ya uongozi au mazingira, kuzungumza kwa uzito mkubwa jambo hilo kutokana na athari zake kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Aidha, kutokana na sababu alizosema kama tatizo ni afya ya akili, viongozi wa dini wanapaswa kuhubiri katika nyumba za ibada kwa kuhimiza waumini wao wakapimwe na kupatiwa ushauri wa kisaikolojia. Pia aliwakumbusha viongozi wa siasa kulizungumzia suala hilo kwa undani na kuchukua hatua zinazostahili.

Kama alivyosema Mtaka, kuna umuhimu mkubwa wa kila mtu kusimama katika nafasi yake kukomesha vitendo hivyo kwa sababu vina athari kubwa kiuchumi na kijamii. Wakati suala la uwekezaji na maendeleo ya viwanda likipewa kipaumbele, kuendelea kwa vitendo hivyo kunaweza kukwamisha wawekezaji kuweka mitaji yao, hivyo kusababisha taifa kushindwa kutimiza azma yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Tuache dhana potofu, tuchukue hatua ugonjwa kifua kikuu upo

**TANZANIA** inakadiriwa kuwa na wagonjwa 130,000 kila mwaka ambao inasemekana wanasumbuliwa na ugongwa wa kifua kikuu au TB na kuifanya nchi kuwa ya 30 kati ya zile zenye ugonjwa huo duniani.

Hayo yamewahi kubainishwa mjini Morogoro na mmoja wa washauri wa mtandao wa wanaopambana na ugonjwa huo kuwa katika idadi hiyo wapo wasiojua kuwa wanao na wengine hawajaanza dozi.

Kifua kikuu kinatajwa kuwa ni moja ya magonjwa hatari yanayoendelea kunyemelea nchi zinazoendelea ikiwamo Tanzania, hivyo kuna haja kila mmoja kuchukua hatua za kunusuru afya yake.

Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na ugonjwa huo, ikiwamo kuwafikia na kuwaweka katika matibabu wenye uhitaji wa huduma ya matibabu ya TB, lakini jamii yenyewe nayo ni vyema ikachukua hatua badala ya kusubiri hali iwe mbaya.

Wako baadhi ya watu wanapoumwa huamini kuwa wamelogwa na hivyo hawaendi hospitalini kupata tiba badala yale wanakwenda kwa waganga wa kienyeji, kitendo ambacho husababisha hali zao kuwa mbaya zaidi.

Inawezekana kundi hilo ni la wale wasiojua kuwa wana ugonjwa huo na hata ambao hawajaanza dozi, huenda ndio hao wanaoamini kuwa wamelogwa na kumbe hakuna ukweli wowote.

Kwa mazingira kama hayo, ninadhani ipo haja ya kutoa elimu ya kutosha kwa Watanzania waachane na dhana potofu na kuwa tayari kupima afya ili kama wameambukizwa, basi wapate matibabu haraka.

Wakati mwingine zinaweza kutumika mbinu mbadala za kukabiliana na ugonjwa huo, ikiwamo kuwashirikisha wale waliowahi kuugua ugonjwa huo wakapata matibabu na wakapona, ili wawe mashuhuda.

Ninaamini hao wakitumika kutoa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo, au kuelimisha jamii kujua dalili za ugonjwa wenyewe wanaweza kueleweka zaidi na kuwafanya watu kuwa tayari kupima afya.

Vilevile, watu hao wanaweza kutumika pia kuwapelekea wagonjwa dawa majumbani. Njia hiyo itasaidia kuwapunguzia wenye TB safari za kwenda na kurudi katika vituo vya kutolea dawa.

Kwa kutumia njia hiyo, kunaweza kuwa na matokeo chanya katika kukabiliana na TB, kwani mbali na kuwapunguzia wagonjwa safari za kila siku, wanaweza pia kuachana na dhana potofu kuhusu ugonjwa huo.

Lakini pia kuwapelekea dawa wagonjwa nyumbani, kunaweza kukaibua wengine zaidi ambao hawataki wajulikane, kwani wanaweza kuwa huru kupima afya zao kupitia kwa watu hao wanaojitolea kutoa huduma.

Huduma ya kupima na matibabu ya kifua kikuu ni bure, katika zahanati mbalimbali, hivyo hata hao ambao wanawapelekea dawa wanaweza kutoa walimu wazuri na wenye ushawishi mkubwa wa kuwafanya waathirika waende kupata dawa katika zahanati zilizo karibu nao.

Kwa mujibu wa wataalam wa afya, mgonjwa mmoja wa kifua kikuu ambaye hajagundulika na kuwekwa katika matibabu, ana uwezo wa kuambukiza watu kati ya 10 hadi 20 kwa mwaka.

Hiyo ni hatari iwapo jamii haitachukua hatua za haraka za kukabiliana na ugonjwa huo kwa njia ya kupima afya mapema badala ya kuchukulia kuwa ni uchawi na kumbe hakuna ukweli wowote.

Katika ufafanuzi wa wataalam wa afya ni kwamba ugonjwa huo husababishwa na bakteria wanaoitwa 'Mycobacterium tuberculosis', na kwamba unaambukizwa kwa njia ya hewa na hushambulia zaidi mapafu.

Wanataja dalili za TB kuwa ni kikohozi kisichoisha, uchovu na kuishiwa kwa nguvu mwilini, kupoteza uzito, kupoteza hamu ya kula, kutokwa na jasho hata wakati kuna baridi, maumivu ndani ya kifua, kuishiwa na pumzi na mate yaliyo na damu au kukohoa damu.

Kwa hiyo jambo la muhimu ni kila mmoja kuchukua hatua za kujikinga au kupata matibabu ya ugonjwa huo na kuweka pembeni dhana zote potofu zinazochangia kuendelea kuwapo kwa TB nchini.

## FIKRA MBADALA

# *Ufalme, usultani viongozi upinzani unaviua vyama vyao*



Pascal Mayalla

NIMESOMA taarifa ya kuchaguliwa tena Prof. Ibrahim Lipumba kuwa Mwenyekiti wa Chama cha CUF, ukiwa ni mwaka wake wa 30 kuwa katika nafasi hiyo. Pia Mzee John Cheyo ni Mwenyekiti wa UDP tangu kimeanzishwa zaidi ya miaka 30 sasa.

Aidha, Freeman Mbowe ni Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa miaka 20 sasa. Japo katiba za vyama vyao hazina ukomo wa madaraka, sasa ni wakati mwafaka zifuate katiba ya nchi kwenye kipengele cha ukomo wa uongozi kuwa mwisho ni vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Mtu akimaliza anapisha wengine hata kwenye ubunge na udiwani na uongozi wowote wa kuchaguliwa. Kazi ya vyombo vya habari ni kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha na kikubwa zaidi, kusaidia. Kama kuna kitu unakijua na unaona kinafanyika ndivyo sivyo, unajitolea kusaidia kuwaelimisha wengine kuhusu kitu hicho. Hiki ndicho ninachofanya kwenye makala zangu, kuwaelimisha wengine kile nilichobahatika kukifahamu. Elimu hii naitoa humu bure, kupitia makala zangu ambazo zinachapishwa kwenye gazeti la Nipashe kila Jumapili.

Kwa vile makala ya leo ni kuhusu vyama vya siasa, naomba kutangaza maslahi yangu kwamba mimi ni kada wa chama cha siasa lakini ninapoandika hapa, siandiki kama kada wa chama chochote bali Mtanzania Mzalendo, ambaye ni mwandishi wa habari niliyedumu kwenye chumba cha habari kwa zaidi ya miaka 30. Pia ni mwanasheria na wakili wa kujitegemea, hivyo ukinisoma kwa mawazo fungamano, hutaiona dhima ya andiko hili na elimu ninayoitoa, hivyo nakushauri unisome ukiwa na mawazo huru.

Msingi mkuu wa nchi yetu ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) ya Mwaka 1977. Kwa mujibu wa katiba yetu, kitu muhimu kuliko kingine chochote, kwanza ni nchi, pili ni mwananchi. Mwananchi ndiye mwenye nchi, ndiye mwenye katiba na ndiye muhimu kuliko kitu kingine chochote.

Mwananchi ametengeneza katiba yenye dhima na dhamira. Dhima ya mtunga katiba, mwananchi ndiye kila kitu na ndiye mwenye nchi, mwenye katiba, mwenye sheria. Anamwajiri Rais wa JMT kupitia kura yake na kumlipa mshahara kupitia kodi yake, hivyo Rais ni mtumishi wa mwananchi, sambamba na mihimili yote mitatu ya dola.

Ibara ya 5 ya katiba, imetoa haki kwa mwananchi kumchagua kiongozi anayemtaka na ibara ya 21 imetoa haki ya kila mwananchi kugombea nafasi yoyote ya uongozi. Haki hizi mbili za kuchagua na kuchaguliwa ni haki kuu za msingi. Mtu akishachaguliwa na wananchi, haiwezekani kikatokea kinyangarika kingine chochote, kikawa na mamlaka ya kumzuia kuwatumikia wananchi.

Serikali yetu kupitia bunge letu tukufu, ilichomekea kipengele batili ndani ya katiba yetu kwenye ibara ya 39 na ibara ya 67, ambazo zimepora zile haki kuu mbili za msingi za kuchagua na kuchaguliwa na kuzikabidhi kwa kitu kinachoitwa chama cha siasa!

Sasa mwananchi hana tena uhuru wa kumchagua kiongozi anayemtaka, hivyo analazimishwa kumchagua kiongozi atakayeletewa na chama cha siasa! Pia Mtanzania hana tena uhuru wa kugombea uongozi, analazimishwa lazima kwanza ajiunge na chama cha siasa, kimdhamini ndipo aruhusiwe kugombea! Lakini viongozi ndani ya vyama vya siasa, wanajigeuza wafalme na masultani kwa kung'ang'ania madaraka. Japo vyama vya siasa ni mali ya wanachama na kuhudumiwa na michango ya wanachama, kwa Tanzania, vyama vya siasa ni vyama binafsi vya wanachama, wakati tu wa kuanzishwa, lakini vikishaingia kushiriki uchaguzi na kushinda, hali inakuwa tofauti. Hali inabadilika kutoka vyama binafsi vya wanachama na kuwa vyama vya umma wa wananchi ndiyo maana vinalipwa ruzuku ya serikali ambazo ni fedha za wananchi.

Fedha za serikali ni fedha za wananchi. Yeyote anayelipwa kwa fedha za wananchi, yaani fedha za walipakodi kutokana na kufuatia viongozi wa vyama hivyo kuchaguliwa na wananchi, kushika uongozi wa serikali za mitaa, udiwani, ubunge hadi urais, waliowachagua ni umma wa Watanzania na si wanachama wa chama pekee. Kwahiyo vyama vyote vya siasa vyenye viongozi waliochaguliwa na wananchi ni vyama vya umma.

Kutokana na hali hiyo ya vyama vya siasa kuwa vya umma, katiba za vyama vyote zilipaswa kuendana na katiba ya nchi kwenye ukomo wa uongozi wa juu na uamuzi wowote wa chama kuhusu uchaguzi, lazima uzingatie maslahi ya umma na si matakwa ya viongozi wake. Kiukweli, baadhi ya viongozi wa baadhi ya vyama vyetu vya siasa ni watu mufilisi kisiasa wenye ubinafsi uliopitiliza. Unaongozaje chama kwa miaka 30 au 20 na unataka tena kuendelea? Lengo la chama cha siasa ni kushika dola, hivyo viongozi wanaogombea nafasi mbalimbali kwa lengo la kushika dola (urais), jimbo (ubunge), kata (udiwani) na mitaa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, hivi vyama vyenye viongozi ving'ang'anizi, vinazidi kusinyaa. Mungu anapomchukua kiongozi mkuu, vyama hivi vinaishia kujifia.

Iko wapi ile CUF ngangari ya jino kwa jino, wapi TLP, wapi NCCR Mageuzi, iko wapi ile DP yenye wabunge machachari? Huwezi kuamini ile CHADEMA yenye wabunge karibu 100, leo ni ya kuwa na mbunge mmoja halafu mwenyekiti baada ya kukaa miaka 20, bado anataka tena ili akafanye nini?

Kwa vile vyama vya siasa ni vya umma, viongozi wa vyama wana wajibu wa kuviendesha kwa kutanguliza mbele maslahi ya umma na si maslahi binafsi. Watanzania tusiruhusu viongozi masultani na wafalme ndani ya vyama vyetu vya siasa. Kwa ubinafsi wa viongozi wao, badala ya kuviimarisha, wana viangamiza.

**+255 754 270403**

## KONA YA AFYA

# *Namna ya kuepuka vidonda vya tumbo wakati wa sikukuu*



Na Dk. Mabula Budodi

DAKTARI nimekuwa sina raha kabisa. Kila ninachokula najisikia vibaya na tumbo linauma sana hasa nikila vitu vya kuchachuka ndiyo inakuwa mbaya zaidi.

"Nikila vyakula kama dagaa, maharage, viazi, ndizi za kupika, pilipili, ukwaju, kutumia limao, chungwa, embe navyakula vilivyoungwa na mafuta mengi na nyanya, nikila pilau lakini nikila wali mweupe bila viongo hainisumbui.

"Lakini nikila papai, tango, tikiti, parachichi na vyakula vya michemsho sipati shida kabisa. Kwa kweli hata hamu ya kula siku hizi imepungua. Nazidi kukonda tu na siishi kwa raha kama awali. Yaani hali hii inanifanya naogopa hata kula kabisa."

Ilikuwa kauli ya mtu aliyekuwa akisumbuliwa na vidonda vya tumbo huku akibainisha kuwa amewashirikisha watu wengi kuhusu tatizo lake na wakamwambia kuwa ana ugonjwa huo, hivyo amefika kupima kwanza ajue kama ni kweli.

**UTAMBUZI VIDONDA VYA TUMBO**

Vidonda vya tumbo ni namna ambayo sehemu ya juu ya tabaka la tumbo na utumbo kutengeneza vidonda. Hali hii huanza pole pole bila mtu kujua kama ana tatizo hilo.

Karibu asimilia 70 watu wenye vidonda huwa hawana dalili yoyote inayoweza kuashiria moja kwa moja kama ana vidonda tumboni.

Vidonda vya tumbo pia huweza kusababisha madhara makubwa sana baadaye visipotibiwa. Ni vyema kutambua dalili na kuhudhuria hospitali kwa ajili ya kugunduliwa na kutibiwa tatizo hilo.

**DALILI ZAKE**

Dalili za uwezekano wa kuwa na vidonda vya tumbo ni nyingi lakini zinazoweza kutokea mara nyingi zaidi ni tumbo kuuma sana kwa kukwangua au kuungua moto. Namna hii ya tumbo kuuma huweza kuongezeka maradufu baada ya kula au usiku wa manane mtu akiwa amelala baada ya kuwa ameshakula saa kadhaa zilizopita.

Vidonda vya tumbo la chakula huweza kupata maumivu muda mfupi baada ya kula na vidonda vya tumbo vya utumbo mdogo, husababisha mtu kupata maumivu zaidi saa kadhaa baada ya kula. Mara nyingi maumivu yake huamsha watu usiku wa manane kutafuta msaada wa daktari.

Dalili nyingine za vidonda vya tumbo ni kubeua mara kwa mara, tumbo kunguruma bila kukoma, kichefuchefu kisichoisha hasa zaidi baada ya kula vyakula vya aina fulani, kiungulia kifuani katikati ambacho wengi huita chembe ya moyo, kupata choo cheusi, kutapika damu ambako huweza kusababisha kupungua damu.

Pia hali hiyo inaweza kusababisha mtu kupungua uzito ambao hueleza kuwa unatokana na kutokula vizuri kutokana na maumivu au kupata madhara yanayoweza kusababishwa na vidonda. Vidonda vya tumbo pia vinaweza kusababisha mtu kupata saratani ya utumbo kwa wazee zaidi na watu walio na kinga ndogo ya mwili.

**SABABU ZA VIDONDA VYA TUMBO**

Sababu kadhaa zimekuwa zikihusishwa na uwezekano wa kupata vidonda vya tumbo kirahisi lakini kubwa ni kupata bakteria anayeweza kusababisha vidonda vya tumbo, yaani helicobacter pylori. (H.pylori).

Bakteria huyo hupatikana katika ulaji wa vyakula ambavyo havijapikwa na kuandaliwa kwa usafi, ubora stahiki na unaweza kuambukizwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine na kutumia dawa ya maumivu kwa muda mrefu hasa zisizo na steroidi kama aspirini na blufein.

Sababu nyingine zinazoweza kusababisha vidonda vya tumbo ni kuvuta sigara, kunywa pombe kupita kiasi, kuwa na msongo wa mawazo wa muda mrefu ambao husababisha kuzalisha asidi nyingi tumboni na kutokula chakula na hata kula vyakula vyenye pilipili nyingi sana.

**VIPIMO NA MATIBABU**

Kugundulika kama mtu ana tatizo la vidonda vya tumbo, huhusisha kusikilizwa na daktari na kufanyiwa uchunguzi wa kitaalam kama kupima kipimo cha mpira cha kumeza chenye kamera kuingia tumboni (endoscopy) na picha za X-Ray za tumbo na utumbo baada ya chakula cha 'barium'.

Lakini pia kwa sababu ya bakteria aina ya H.pylori imekuwa sababu kubwa ya kupata vidonda hivi, yapaswa kupima choo kumwangalia mdudu huyo kama yuko tumboni.

Anaweza pia kuangaliwa kwenye damu lakini huonekana vizuri zaidi kwa njia ya choo kutokana na kuambukizwa kwa njia ya mdomo na choo baada ya kula chakula, kunywa maji ambayo yana mdudu huyo ambayo yameambukizwa tayari na mdudu wa aina hii.

Njia nyingine ni kuandaliwa chakula na mtu mwenye mdudu huyo kama hajanawa mikono baada ya kutoka chooni .

Mtu anaweza kuwa na mdudu ambaye anaweza kusababisha vidonda vya tumbo, yaani H.pylori lakini asiwe na vidonda vya tumbo kama wengi ambavyo hudhania kukutwa na mdudu huyo ndiyo kuwa na vidonda vya tumbo.

Matibabu ya vidonda vya tumbo huhusisha matumizi ya 'antibiotiki' kwa ajili ya kumwondoa mdudu ili asisababishe vidonda hivyo, kutumia dawa ya kupunguza asidi tumboni na hata kubadili mfumo wa maisha kama kutokunywa pombe, kutokuvuta sigara, kuzingatia kula sehemu isiyo safi na salama na kunywa maji safi na salama.

Ili kutambua kama mtu ana vidonda vya tumbo, anapaswa kumwona daktari ili kupima na kupata tiba na ushauri. Mtu anapaswa kuzingatia hilo ili kuepuka madhara ya vidonda vya tumbo hasa msimu wa sikukuu.

**•Dk. Budodi ni daktari wa binadamu anapatikana Dar es Salaam. Unaweza kuwasiliana naye kwa namba 0710 980096 au barua pepe mabulabododi@gmail.com**

# Serikali kubuni mikakati kuimarisha utalii

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itaendelea kubuni mikakati ya kuimarisha sekta ya maliasili na utalii kwa kuwa ni nguzo muhimu kwa uchumi wa taifa.

Majaliwa aliyasema hayo juzi alipozindua Tuzo za Uhifadhi na Utalii katika Ukumbi wa Hoteli ya Mount Meru jijini Arusha.

Tuzo hizo zinalengo la kuchochea ushindani kati ya wadau wa sekta ya maliasili na utalii nchini.

Alisema maliasili na utalii ni chanzo kikubwa cha mapato ya taifa kwa kuwa ni sekta inahusisha shughuli nyingi za kiuchumi.

"Sekta hii peke yake inachangia asilimia 21.5 katika pato ghafi la taifa ambapo asilimia 17.2 ni utalii, asilimia 4.3 ni misitu na nyuki," alisema.

Pia alisema sekta hiyo inachangia asilimia 30.9 ya mapato ya fedha za kigeni ambapo asilimia 25 yanatokana na utalii na asilimia 5.9 ni misitu na nyuki.

Katika hatua nyingine, Majaliwa alisema juhudi za dhati na maono makubwa ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kuiendeleza sekta ya maliasili na utalii yamesaidia kuongeza idadi ya watalii wa kimataifa kwa asilimia 96 kutoka 922,692 mwaka 2021 hadi 1,808,205 mwaka 2023.

"Jitihada za Rais Samia zimesaidia pia kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii wa kimataifa kwa asilimia 68.2 kutoka dola za Marekani bilioni 2.0 mwaka 2021 hadi bilioni 3.4 mwaka 2023," alisema.

Majaliwa pia aliiagiza Wizara ya Maliasili na Utalii kuweka vigezo vya wazi na vinavyojulikana vya uteuzi na upokeaji wa tuzo.

"Vigezo hivyo, pamoja na mambo mengine, viwe vinavyozingatia ubora katika uhifadhi wa mazingira, huduma za utalii, usimamizi wa hifadhi za wanyama na uendelezaji wa maeneo ya utalii," alisema.

Waziri wa Maliasili na Utalii Balozi Pindi Chana, alimshukuru Rais Samia kwa namna anavyojitoa katika kuhakikisha sekta ya maliasili na utalii inaendelea kukua kwa kasi.

Aliongeza kuwa wizara hiyo imekuwa na mikakati mbalimbali ya kuimarisha uhifadhi na kuendeleza utalii ikiwemo kutumia teknolojia mbalimbali pamoja kuendeleza Programu ya Tanzania - 'The Royal Tour' na kuibua mazao mapya ya utalii ili kuongeza idadi ya watalii na mapato yatokanayo na shughuli za utalii.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipokea tuzo kutoka kwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Prof. Palamagamba Kabudi, kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwa Kiongozi mwenye maono katika maendeleo ya uhifadhi na utalii wakati wa Uzinduzi wa Tuzo za Uhifadhi na Utalii, katika Ukumbi wa Hoteli ya Mount Meru, Arusha juzi. **PICHA:OWM**

# Tanzania, Saudi Arabia kuimarisha ushirikiano nishati

**Na Mwandishi Wetu, Riyadh,** SAUDI ARABIA

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, amesema Tanzania itaendelea kushirikiana na Saudi Arabia katika kuimarisha sekta ya nishati hususan katika mafuta na gesi, nishati safi ya kupikia na nishati jadidifu.

Kapinga aliyasema hayo juzi alipokutana na Naibu Waziri wa Nishati wa Saudi Arabia, Mhandisi Mohammed Albrahim, mjini hapa.

Alisema Tanzania imekuwa ikishirikiana na nchi hiyo kwa muda mrefu katika biashara ya mafuta na maeneo mengine ya maendeleo, hivyo uhusiano huo utaendelea kuimarika zaidi kwa kuwa mahitaji ya nishati yanazidi kuongezeka.

Pia alisema uwekezaji zaidi unahitajika katika kuendeleza sekta ya mafuta ikiwamo mafuta na gesi asilia, nishati jadidifu na nishati safi ya kupikia.

"Uhusiano wa Tanzania na Saudi Arabia katika sekta ya nishati ni wa muda mrefu. Nchi hizi mbili zimekuwa na lengo la kuboresha ushirikiano wao katika kuendeleza sekta ya nishati," alisema Kapinga.

Pia alisema Tanzania kama nchi inayoendelea, inahitaji kuimarisha zaidi miundombinu yake ya nishati katika maendeleo, hivyo imekuwa ikishirikiana na nchi zenye uzoefu mkubwa katika sekta hizo ili kupata matokeo chanya kwa kuwa nishati ni msingi mkuu wa maendeleo.

Alisema Saudi Arabia imekuwa ikijulikana kwa uwezo wake mkubwa katika uzalishaji wa mafuta na gesi na imekuwa ikiwekeza katika maeneo mbalimbali ya Dunia ikiwemo Afrika Mashariki.

Kapinga alisema kwa upande wa Tanzania yenye rasilimali za gesi asilia na viashiria vya uwapo wa mafuta, inapata uzoefu, ujuzi na teknolojia kutoka Saudi Arabia katika kuchimba, kusafisha na kusafirisha mafuta na gesi pamoja na kuimarisha miundombinu ya rasilimali hizo.

Aidha Kapinga alisema kuimarika kwa sekta ya nishati nchini kutaiwezesha nchi kusambaza umeme utakaozalishwa nchini kwa nchi jirani ambazo zimeonyesha nia ya kuhitaji nishati hiyo.

Naibu Waziri wa Nishati wa Saudi Arabia, Mhandisi Mohammed Albrahim, alisema nchi yake inajipanga kuwekeza zaidi katika ujenzi wa miundombinu ya barabara, utunzaji wa mazingira na kuwekeza zaidi katika sekta ya nishati hususan mafuta na gesi, nishati jadidifu na nishati safi ya kupikia.

Alisema pamoja na kwamba wamegundua mafuta mengi, wanajipanga kuendana na sera za kidunia kwa kuwekeza katika nishati safi ambayo inahifadhi mazingira.

Naibu Waziri huyo aliongeza kuwa Saudi Arabia inatambua juhudi zinazofanywa na Tanzania kupitia Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kinara katika kutekeleza ajenda ya nishati safi ya kupikia.

## Ataka kila wilaya kuwa na mwenyekiti wa baraza la ardhi

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

MRATIBU wa kampeni ya msaada wa kisheria ya 'Mama Samia Legal Aid' Mkoa wa Mara, Laurent Buliro, amesema kuna haja ya kuongeza wenyeviti wa mabaraza ya ardhi na nyumba ili kupunguza mrundikano wa mashauri.

Alisema hayo juzi alipowatembelea wananchi wa mtaa wa Mtakuja 'A', Kata ya Mwisenge mjini hapa kwa ajili ya kutoa elimu ya sheria juu ya migogoro ya ardhi, ndoa, mirathi na sheria ya unyanyasaji wa kijinsia.

"Tumepewa maelekezo na Wizara ya Katiba na Sheria kufanya utafiti. Licha ya kwamba tayari wizara imeanza kuchukua hatua mbalimbali za kupunguza mashauri ya ardhi, kwa sasa njia pekee ni kuongeza wenyeviti wa mabaraza ya ardhi na nyumba walau kila wilaya awepo," alisema Buliro.

Alisema kwa sasa maeneo mengi mwenyekiti mmoja anahudumia zaidi ya wilaya moja, akitolea mfano anayehudumia wilaya ya Musoma pia anahudumia Butiama na awali alikuwa akihudumia Bunda na Serengeti.

Wakili wa kujitegemea kutoka Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), Emmanuel Baraka, alisema mwenyekiti mmoja wa mabaraza ya ardhi anayehudumia mashauri 2,000 ikitokea amepata matatizo ya kiafya, mashauri hayo yatasogezwa katika miezi ya mbele, hivyo kuna haja ya kuongeza idadi yao.

"Mabaraza haya yako chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ambayo ndiyo hii inazunguka sasa lakini mwenye wajibu wa kuongeza ni Msajili wa Mabaraza akishauriana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi," alisema Baraka.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Aloyce Masatu, alisema lengo la mkutano huo ni kuwafikishia wananchi wa eneo hilo elimu ya kisheria sambamba kutokana na migogoro ya ardhi kukosa ufumbuzi kutokana na baadhi ya wananchi kushindwa kumudu gharama za mawakili.

Kampeni hiyo ambayo ilitamatika juzi mkoani hapa, imewapatia wanasheria wa kusimamia mahakamani bure wananchi wasio na uwezo wa kumudu gharama.


# MAISHA

DESEMBA 22, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili

HARUSI

Ukurasa 12






## SHONA NGUO UPENDEZE

Ukurasa 13

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| C | O | W | | H | |
| A | | | | O | |
| T | I | G | E | R | |
| S | | O | | S | |
| | | A | P | E | S |
| B | A | T | | | |


## FUMBO TOTO

Haya, hebu tuone umahiri wako wa somo la Kiingereza shuleni; jaza majina haya ya wanyama kwa Kiingereza katika fumbo letu.

KUNGURU, POPO, SUNGURA, PAKA, MWEWE, PANYA, SWIRA, DUBU



## TOA TOFAUTI 5





## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

MATOKEO YAKO YA KUFUNGA SHULE YAMEONESHA UMEPATA UFAULU WA ALAMA B. TUMIA LIKIZO HII KUTAFUTA NJIA YA KURUDI ALAMA A.




Alichokifanya daktari

TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake “usiku mwema mwanangu”

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao “Pata njozi njema mwanetu”

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuambia “usiku mwema mpendwa wetu”

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia “Kesho uamke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani”

**SWALI**

Makaa ya mawe yanapatikana wapi hapa Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Ndoa nyingi huvunjika muda mfupi

KARIBU msomaji tumulike talaka. Ndoa ni nyingi hasa majira haya ya mwishoni mwa mwaka na talaka pia ni nyingi. Hebu sikia majadiliano kikao kimoja cha maandalizi ya harusi hivi majuzi. Nyingi hazidumu, zinavunjika baada ya muda mfupi, ni kwa nini?

Ziko sababu mbalimbali ambazo wameeleza kwamba zinachangia ongezeko la talaka pamoja na ukweli kwamba ndoa zingine zimefanyika kwa maandalizi yenye gharama kubwa sana. Ziko zinazoanzia Sh. 500,000 hadi milioni 15 na pengine zaidi kwa hapa kwetu. Ulaya huko ndiyo usiseme kwani huwa ni kufuru kutegemeana na uwezo wa familia husika.

Naam. Ndoa ni furaha, ndoa ni maridhiano kati ya mke na mume. Liko swali lilijitokeza wakati tunazungumza na jamaa fulani walioujumuika katika kikao kile cha harusi. Kwa nini mke na mume huachana baada ya kuwa wamejenga uhusiano kwa muda mrefu hata kufikia kufunga pingu za maisha?

Jibu ya swali hili ni pana sana. Msomaji wangu nitajaribu kulijibu kupitia maeneo machache tuliyojadili kwa muda mfupi wakati wa mazungumzo yale. Moja ya sababu zilizotajwa ni tatizo la kiuchumi.

Tatizo hilo nililianzishia mjadala mimi. Nikasema kwamba ziko ndoa ambazo ama huvunjia au wanandoa kutengana kama si kuachana kabisa kutokana na uchumi wa familia kuyumba.

Mwanamke anaweza kuolewa na mwanamume tajiri na maisha yakawa murua. Lakini kama ambavyo uchumi wa nchi au wa dunia unavyoyumba kupata misukosuko, pia uchumi wa familia unaweza kuyumba. Hapo ndipo mitafaruku huanzia.

Hali hii haizikumbi familia tajiri tu bali hata zile za kawaida. Jamaa anafanya biashara ndogo ndogo. Wakati mwingine mtaji hukata na hivyo mtiririko wa huduma nyumbani kuanza kuwa wa mashaka. Milo mitatu inashindikana inashuka hadi mlo mmoja.

Ada ya mtoto au watoto inaanza kuleta shida, hapa kufikia watoto hawaendi shule. Matokeo yake baba au mama anaanza kwenda kuhemea misaada. Kufikia hapo, mama mmoja akadakiza;

"Umesema ukweli. Kuyumba kwa uchumi wa familia kumeleta shida sana katika baadhi ya familia. Kumechangia msongo wa mawazo kwa kinamama hata kufikia wengine kuzikimbia kwa muda familia zao kama siyo kutokomea kabisa hasa wale wasiofungwa na mkataba wa ndoa.

"Hata hivyo, pamoja na ukweli huo, hiyo siyo sababu ya kutengana kwa sababu iwe ni baba au ni mama wanapaswa kuwa ngangari na kupambana na mtikisiko huo wa kiuchumi ndani ya famili", alisema mama huyo.

Baba mmoja aliyeshiriki mazungumzo hayo alisema: "Huwa nawashangaa sana kinamama wanaokimbia nyumba zao au wanaofanya vitimbi baada ya kuona waume zao wanayumba kiuchumi.

Mama mwingine akachekesha pale aliposema: "Tuambizane ukweli. Kama mumeo unajua kabisa ana uwezo kifedha, lakini huduma nyumbani ni 'mbofu mbofu', na wakati huo huo unapata uthibitisho kuwa anamjengea mwanamke wa pembezoni nyumba au kamnunulia gari, kwa nini usicharuke na hata ikiwezekana kubomoa ndoa?

Mwingine aliyekuwa pembeni anafuatilia majadiliano yale akajisogeza karibu na kusema: "Niliomba talaka hata kabla ya kumaliza miaka miwili tokea tufunge ndoa ya nguvu na mume wangu. Ni pale nilipogundua kuwa mume yule alishaoa na kuacha wanawake wa nne na mimi ilikuwa ndoa ya tano. Hakunielewa kwa nini nilichukizwa kiasi kile." Baada ya kusema hayo aliomba kuvamia mazungumzo.

> **Ada ya mtoto au watoto inaanza kuleta shida, hapa kufikia watoto hawaendi shule. Matokeo yake baba au mama anaanza kwenda kuhemea misaada. Kufikia hapo, mama mmoja akadakiza;**

Sababu zingine ni pamoja na unywaji wa pombe kupita kiasi hasa kwa upande wa mwanaume, hali ambayo inasababisha huduma nyumbani kuwa hafifu kuanzia chakula na hata mahusiano ya ndoa. Haki ya ndoa inapolega lega, kinamama wengine hudai talaka ili wakajiridhishe kwingineko. Uaminifu unapotoweka ndani ya nyumba talaka hunyemelea.

Pia familia kugawanyika kikazi kumechangia talaka. Baba anafanya kazi Dar na mkewe kahamishiwa ualimu Kigoma. Wawili hao ambao ndio kwanza wana watoto wawili, utengano huo utakuwa na tija gani kwao? Kama siyo kuruhusu michepuko (nyumba ndogo) ni kitu gani?

Talaka si jambo lenye afya bali ni tatizo linalochipua matatizo mengine kama vile kugombania mali zilizochumwa pamoja na wakati mwingine kugombania watoto na wakati mwingine wazazi hudiriki kugawana.

***Je, una maoni au kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe 0715268581. Namba hii iko pia WhatsApp.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Mbowe, Lissu walivyoiweka CHADEMA juu ya kaburi

VITA vya madaraka kati ya nguli wa siasa za upinzani nchini Tanzania, Freeman Mbowe na mwanasiasa mwenye damu ya harakati, Tundu Lissu, inaweza kuwa na sura tofauti, baada ya uchaguzi wa viongozi wakuu wa chama hicho kutamatika Januari, 2025.

Wako wanaouchukulia uchaguzi huo unaovuta hisia za wengi kama zimwi. Uko msemo wa waswahili usemao, zimwi likujualo halikuli likakwisha.

Naweza kusema hivyo kutokana na mnyukano wa kihafidhina na makundi unaoendelea kati ya kambi ya Mbowe na Lissu.

Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa anayemaliza muda wake, Freeman Mbowe, anakabiliwa na kibarua kigumu cha kutetea nafasi yake kwenye uchaguzi ujao dhidi ya makamu wake, Tundu Lissu.

Yanayoendelea huko yanaashiria kuwapo kwa upinzani usio na umoja. Ukweli ni kwamba mpasuko kati ya Mbowe na Lissu umekuwa ukiongezeka, huku Lissu akimtuhumu Mbowe kwa kumzuia kufanya mikutano ya hadhara na vikao vya ndani vya chama.

Mgogoro huu ndani ya CHADEMA unaonesha wazi ukosefu wa umoja ambao ni muhimu kwa chama chochote kinachotamani kuongoza taifa.

Badala ya kushirikiana na kuonyesha sera ambazo zingeweza kuwafaidisha wananchi, viongozi wa CHADEMA wamejikita kwenye mvutano wa nguvu na ushawishi, bila kujali maslahi ya umma.

Swali unaloanza kujiuliza ni maeneo gani yanayompa nguvu Freeman Mbowe? Kimsingi, huyu ndiye ameshiriki kutengeneza kizazi cha wanasiasa wengi kutoka ndani na nje. Wako vijana walioingizwa kwenye chama wakiwa hawana ujasiri au ufahamu wa kutosha katika siasa.

Katika kundi hili, amevutia na kusajili vijana ambao sasa wanaonekana wazoefu katika siasa. Ni rahisi kuona baadhi yao wakiweka wazi juu ya kumpigania Mwenyekiti huyo na bila shaka wapo tayari kulipa fadhila.

Baadhi ya vijana hao wameshinda uchaguzi wa ndani katika nafasi za uenyekiti kwenye majimbo mbalimbali wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kanda ya Pwani, Boniface Jacob 'Boni Yai'.

Katika suala la fursa, hakuna ubishi kwamba sehemu kubwa ya wajumbe wanaohusika kupiga kura kwenye uchaguzi huo wanatokana na uongozi wa Mbowe.

Wajumbe 1,200 ni matokeo ya uongozi wake kwa kipindi kilichopita. Je watakuwa tayari kuachana na siasa za Freeman Mbowe? Swali gumu sana kwao. Hata nguvu ya kiuchumi.

Tazama aina ya wenyeviti wa vyama vya siasa nchini, wamekuwa na dhaifu katika nguvu za uchumi. Wengi wao walikuwa wanasiasa ambao hawakuwa na uwezo mkubwa kiuchumi.

Duru za siasa zinasema kuwa sababu ya nguvu ya kiuchumi, ina mchango mkubwa kumpa ushindi Freeman Mbowe. Mnamkumbuka bingwa wa siasa za kaskazini, marehemu Philemon Ndesamburo maarufu kama 'Ndesa Pesa' alivyokuwa na ukwasi?

CHADEMA inamtaka mtu aina yake ambaye ni Mbowe. Vyama vya upinzani vinahitaji si viongozi wazuri pekee, bali pamoja na uwezo wa kiuchumi. Kwa mtazamo wa CHADEMA, anayegombea Uenyekiti wa chama chao angalau awe imara kiuchumi.

Mitazamo ya wana CHADEMA ni dhahiri inaonekana wanatamani kama kuna mwanasiasa mwenye nguvu za kiuchumi kumzidi Freeman Mbowe, wakamfikiria hata kama hatachaguliwa.

Wanaoijua siasa ya Afrika Mashariki ya sasa, nguvu ya uchumi ndiyo inayowabeba wanasiasa wa upinzani. Mfano halisi ni Moise Katumbi Chapwe wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Kwa matukio ya kuumizwa, Lissu na Mbowe, wana historia hiyo. Mmoja alipigwa risasi nyingi na mwingine alishtakiwa kwa ugaidi. Eneo hili kila mmoja anaweza kulitumia kuombea kura za huruma kwa wajumbe.

Mathalani, Mbowe anaweza kutumia kampeni zake kueleza namna alivyoitwa na kufunguliwa mashtaka ya ugaidi. Lissu pia atasema aliumizwa kwa risasi. Wote wawili watasema walikuwa wanakipigania chama.

Ukomo wa uongozi ni eneo muhimu ambalo linatakiwa kuangaliwa kwa mapana, endapo utaratibu wa sasa unafaa au haufai na rasilimali za chama.

Ajenda za Lissu zinagusa zaidi suala la fedha na uendeshaji wa chama hicho kikuu cha upinzani nchini.

Suala la fedha za chama ni jambo la muda mrefu ambalo limekuwa likitumika kumkosoa mwenyekiti huyo juu ya udhibiti na usimamizi wa mapato. Mara kwa mara wamepata 'hatichafu' kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Hata yanayoitwa 'maridhiano' Mbowe ana maswali mengi ya kujibu. Vita hivi vya madaraka, visa na umimi, kwamba huyu kaongoza kwa miaka 21 usiigawe CHADEMA.

Kumbukeni mmeijenga kwa jasho na damu hadi hapo ilipofikia na hakuna mkubwa kuliko CHADEMA. Nakuacha na tafakuri hii, ni kwa nini ni vigumu kwa baadhi ya viongozi wa Afrika kuondoka madarakani?

**•Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI



Mtangazaji wa EFM, Tunu Hassan, akiwa na mumewe baada ya kufunga ndoa jijini, Dar es Salaam hivi karibuni. Sherehe ya kumpongeza itafanyika kesho kwenye Ukumbi wa MayFair Plaza.

MITINDO

Na Moshi Lusonzo

# SHONA NGUO UPENDEZE



USHONAJI wa nguo ni moja ya jambo linalofurahisha wengi kutokana na kutoa nafasi kwa mtu kuvaa nguo anayoipenda.

Hata hivyo, kuchagua kitambaa kinachofaa kwa ajili ya kushona nguo imekuwa tatizo baada ya idadi kubwa ya watu kutokuwa na ufahamu aina ya vitambaa.

Kukiwa na aina nyingi tofauti za vitambaa ni muhimu kuelewa vipengele muhimu vinavyochangia kuchagua kitambaa kinachofaa zaidi.

Vitambaa vya utengenezaji wa mavazi hufumwa au kuunganishwa, na vinaweza kutengenezwa kwa hariri, nailoni, polyester, spandex, rayon, na zaidi.

Vitambaa vinavyotengenezwa na vifaa tofauti na michakato ya utengenezaji vitakuwa na mng'ao tofauti, unene, umbile na uvutano.

Kitambaa cha Satin

Satin ni kitambaa laini, kinachometameta ambacho kimetengenezwa kwa hariri, polyester, au mchanganyiko wa nyuzi hizo mbili.

Kitambaa kina mwonekano wa kifahari. Kwa kawaida ni kitambaa cha kukichagua kwa ajili ya vazi rasmi na nguo za hafla maalum.

Moja ya sifa kuu za satin ni uwezo wake wa kuakisi mwanga. Ubora huu huipa satin mng'ao wa kipekee, ambao unaifanya kuwa chaguo maarufu kwa nguo za sherehe na gauni za harusi.

Kitambaa cha Chiffon

Chiffon ni aina ya kitambaa tupu, chepesi ambacho hutumiwa mara nyingi katika tasnia ya mitindo kuunda mavazi ya jioni ya kifahari na ya kuvutia.

Moja ya sifa za chiffon ni uwazi wake, ambao unaruhusu mtu kupendeza.

Kitambaa hiki kinatumika kutengeneza nguo za mitindo mbalimbali kama gauni la jioni hadi blauzi za kawaida na sketi.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# Kama una ngozi kavu epuka haya..

NGOZI kavu inaweza kukufanya ukose raha kutokana na kuwasha na kupauka mara kwa mara, kupata mikunjo ya ngozi na hata kupata vidonda.

Aina hii ya ngozi husababishwa na baridi, pia baadhi huzaliwa nayo.

Kama una ngozi ya aina hiyo basi haya ni mambo matatu ya kuyaepuka kufanya.

**Usioge maji ya moto**

Epuka kuoga maji ya moto mara kwa mara, kwani kunaweza kufanya mafuta asili yanayolainisha mwili kukauka.

Katika kuepuka tatizo hili ni vyema ukatumia maji ya uvuguvugu au baridi kwa kuoga au kunawa.

**Usitumie vipodozi**


Vipodozi vyenye asili ya kilevi (Alcohol) husababisha ngozi kuzidi kuwa kavu.

Wakati wa kwenda kununua vipodozi vyako hakikisha unasoma maelezo na kujua kiasi cha kilevi kilichopo kama ni nyingi usichukue, nunua yenye kiasi kidogo.

**Usisugue au usioshe**

Kuosha ngozi na sabuni mara nyingi ni njia ya mojawapo ya kufanya ngozi kuwa kavu.

Ngozi kavu iliyokasirika huathirika zaidi na maambukizi ya bakteria kwa sababu kuosha mara kwa mara huondosha safu za kinga ya ngozi yako.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Bagia za kunde

KUNDE ni miongoni mwa vyakula vya nafaka ambavyo hutumika katika aina mbalimbali za mapishi.

Miongoni mwa vitafunwa unavyoweza kuandaa kwa kutumia kunde ni bagia ambazo hupikwa kwa mitindo mbalimbali ikiwamo kuzisaga au kuzichemsha kisha kuzikaanga.

Wakati huu wa sikukuu unaweza kutengeneza kunde zako nyumbani na familia ikatumia kama kitafunwa.

**Mahitaji**

Mafuta, vitunguu maji, kotrimiri, kitunguu saumu,kunde robo, pilipili mbuzi moja, tangawizi moja na binzari nyembamba.

Namna ya kupika

Baada ya kuchambua kunde zilizokobolewa au nzima ziloweke kwenye maji kwa saa 12 au zaidi ili zilainike.

Baada ya kulainika vizuri zichuje kisha uendelee na maandalizi ya viungo kitunguu maji, pilipili mbuzi, kotmiri, tangawizi na kitunguu saumu ambapo utaviosha (kwa vinavyohitajika kuoshwa) na kuvikatakata kwa saizi ndogo.



Endelea na maandalizi kwa kuchanganya viungo vikavu na kunde ikiwamo chumvi, manjano, baking soda na vingine unavyopendelea, ongeza viungo vingine ulivyoviandaa awali kisha uvichanganye na usage kwa kutumia blenda.

Unaweza kutumia mawe ya asili ya kusagia au kutwanga na kinu hadi zilainike kabisa na kutengeneza mchanganyiko mzito.

Bandika mafuta jikoni na yakipata moto anza kuchota bagia kiasi kwenye mkono, tengeneza umbo ulipendalo kisha uzikaange mpaka ziwe na rangi ya kahawia.

Wakati unazikaanga hakikisha moto sio mkali sana ili kuepuka kubabua bagia au kuzifanya zisiive kwa ndani.

Baada ya dakika 7 hadi 8 bagia zikibadilika kuwa na rangi ya kahawia zitakuwa tayari kwa kula.

Unaweza kuongeza ladha ya kitafunwa chako kwa kuzitengenezea pilipili ya ukwaju, embe au aina yoyote ile utakayopendelea.

# Pamba mishumaa sikukuu hii

Na Restuta James

PAMOJA na kwamba mishumaa inatumiwa kuleta mwanga ndani ya nyumba, matumizi yake ni zaidi ya hapo, hasa msimu huu wa sikukuu.

Kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka, tovuti kadhaa zinazojihusisha na mapambo ya nyumba, zinaeleza matumizi ya mishumaa.

Mtaalamu wa mapambo, Asajile Brown, anasema mishumaa inapendeza ikitumiwa wakati huu wa sikukuu hasa kwa kuwa ni kipindi cha familia kukaa pamoja.

Anasema mishumaa inaweza kuwashwa kwa lengo la kutakiana heri na mwaka mpya wenye baraka, za kukua kiroho na kimwili kwa wapendwa, akitaja mafanikio ya kifedha, kikazi na kihuduma.

Anasema rangi za mishumaa zinapaswa kuambatana na kusudio la kuwashwa kwake akitaja nyeupe, kijani, njano, zambarau, pinki, dhahabu na fedha.

"Rangi za mishumaa zinatabiri upendo, umoja, uponyaji, amani, ulinzi, heshima, mvuto, furaha, nguvu, urafiki, utajiri, bahati, mwangaza, uchangamfu, afya, malengo na kusafisha mtazamo hasi," anasema.

Anatoa mfano kwamba mishumaa inaweza kuwashwa kwa ajili ya kutakiana mafanikio ya kifedha, kutafuta vilivyopotea na kukuza urafiki.

Aidha, anasema mishumaa pia inaweza kutumika yenye harufu ya manukato tofauti tofauti, yakiwamo ya matunda kama chungwa au limao.

Anasema mishumaa inaweza kuwa na harufu ya viungo vya chakula kama mchaichai, karafuu au mint.

Magreth anasema mishumaa inaweza kuwashwa kwenye bustani au ndani, akishauri kwamba katika msimu wa sikukuu za kuelekea mwisho wa mwaka, ni pambo linaloweza kutumiwa kuweka malengo ya mwaka mpya.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Namna ya kupangilia kabati la vyombo kwa urembo wa nyumba

KABATI la vyombo ni miongoni mwa samani zenye uhitaji mkubwa kwenye nyumba.

Watu waliobarikiwa kujenga au kuishi kwenye nyumba zenye nafasi ya kutosha, kabati huwa ni moja ya vitu muhimu kwao kwa ajili ya kuhifadhia vyombo.

Lakini leo nataka tuzungumzie kazi nyingine ya kabati kwenye eneo la urembo kwenye nyumba.

Kama ilivyo urembo mwingine kwenye nyumba, kabati la vyombo nalo lina nafasi ya kutumikia kama urembo.

Kutumika kwa kabati kama urembo si kwa kuweka maua au urembo mwingineo ndani yake, ni kwa kutumia vyombo hivyo hivyo ambavyo badala ya kutumika kwa ajili ya matumizi ya chakula, pia vitumike kama urembo.

Na ili vitumike kama urembo, kitu cha kwanza lazima kwanza tujue eneo linapopaswa kuwekwa ndani ya nyumba husika.

Jambo lingine lazima kuhakikisha kwamba vyombo vinavyowekwa kabatini ni vile vyenye mvuto au vizuri, usichukue tu vyombo ilimradi na kwenda kuviweka humo.

Hakikisha unazingatia rangi za vyombo vyako vinavyowekwa kabatini, zisiwe zile za kuumiza macho sana na ikiwezekana rangi zake zisipishane sana na zile za vitu vyote vilivyopo kwenye nyumba yako.

Kuwa mbunifu kuvipangilia kwenye kabati ili vilete mvuto, zingatia aina na muundo wa vyombo.

Kama ni sahani, hakikisha unapangilia kuanzia zile kubwa kuelekea ndogo zake, fanya hivyo na kwa glasi, vikombe, bakuli na vinginevyo ambavyo ni vizuri unavyokuwa umeviandaa kwa ajili hiyo.


Kumbuka si lazima viwe vinatumika, vinaweza kuwa maalum kwa urembo tu na vile vya kutumia ukaviweka sehemu nyingine au katika kabati la juu la jikoni.

Na kama uwezo hauturuhusu, unaweza pia ukavitumia, lakini unapomaliza unahakikisha kwamba unavisafisha vizuri na kuvirudisha katika sehemu yake vinapopangiliwa na katika hili ubunifu zaidi unahitajika.

Katika mpangilio unaweza kuamua grasi zikae sehemu yake, au ukaamua kila shefu zikae tatu au nne kwa mpangilio mzuri, au kila aina ya chombo ulichonacho ukakitumia kwa mpangilio maalum katika shefu zote ili 'kunogesha zaidi'.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
MKE WANGU AGIZA MATARUMBETA UNIPONGEZE MUMEO KRISIMASI HII SINA MCHEPUKO!
'MIAKA TISA' KILA MWAKA NAWAAHIDI WAZEE NAWAJENGEA ILA POMBE ZIKINITOKA NSHASAHAU!
JUKWAANI
NINA RAHA NATEMBEA NIKIWA HURU SHETANI KASHINDWA!
NGOJA UZIPATE AKUITE BAR UKATAE!
SIJUI ANAKUJA NA UONGO GANI!
NAMUONAGA KAMA VIDEO!
HIVI PRESHA NA MOYO NA SHINIKIZO LA DAMU KWANI SABABU YAKE NINI?
UNA NYUMBA NDOGO UNAYO-IGHARAMIA INAPIGIWA MISELE?
WEWE! MASUALA YA KUJIKIMBIZA JOGING' KUKATA MAFUTA SIO LAZIMA!
'TUKUPE MAUA'
SIKUKUU HIZI NIMEPATA KIGOLI NIJIANDAE KUTANGAZWA LAIVU "KAFIA GESTI"
HII NI MECHI AU LIGI YA MPIRA?
MDAKO

## HABARI KIMATAIFA

# Dereva agonga watu sokoni, wawili wapoteza maisha

**BERLIN,** UJERUMANI

MTU mmoja amekamatwa baada ya kuendesha gari katika soko la Krismasi katika mji wa Magdeburg, nchini Ujerumani, na kusababisha watu wawili kufariki dunia na wengine 68 kujeruhiwa.

Waziri Mkuu wa Ujerumani alisema hawezi kuthibitisha iwapo idadi ya vifo haitaongezeka kutokana na watu kujeruhiwa vibaya.

Mtu anayeshukiwa kuendesha gari hilo alikamatwa muda mfupi baada ya tukio hilo na ametambuliwa kama daktari mwenye umri wa miaka 50 kutoka Saudi Arabia, ambaye anaishi Ujerumani tangu mwaka 2006. Viongozi mbalimbali duniani wametoa salamu zao za rambirambi wakieleza kusikitishwa na shambulio hilo. Marekani ilisema kuwa tukio hilo linatisha huku Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron akisema ameshtushwa sana.

Ibada ya kumbukumbu ilifanyika katika kanisa kuu la mji huo jana, huku matukio ya kitamaduni yaliyopangwa yamefutwa.

Kulingana na baadhi ya ripoti za habari za Ujerumani, mshukiwa huyo hakujulikana kwa mamlaka kama mfuasi wa itikadi kali za Kiislamu, huku mitandao ya kijamii na machapisho yake mtandaoni yakionesha kuwa alikuwa akiukosoa Uislamu.

Wachunguzi wa tukio hilo hawajaeleza hadharani lengo lake lakini walisema wanaamini kwa sasa kwamba mtuhumiwa alitenda kosa hilo peke yake.

Rais wa Halmashauri kuu ya Umoja wa Ulaya, Ursula von der Leyen, alituma salamu za pole kwa waathirika wa shambulizi hilo.

Von der Leyen aliandika kwenye mtandao wa kijamii wa X akisema yuko pamoja na jamaa na marafiki wa waathirika wa shambulizi hilo huku akiwashukuru polisi kuchukua hatua za haraka na walitoa huduma ya uokoaji.

Waziri wa Mambo ya Ndani, Nancy Faeser na Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz pia walitarajiwa kutembelea eneo hilo jana. Scholz aliandika kwenye mtandao wa X akisema "Fikra zangu ziko na waathiriwa na familia zao. Tunasimama pamoja na watu wa Magdeburg. Shukrani zangu ziwafikie jeshi la uokoaji waliojitolea kwa hali na mali katika saa iliyojaa mashaka makubwa."

**BBC**

## Russia yadungua droni 19

**MOSCOW,** RUSSIA

WIZARA ya Ulinzi ya Russia, imesema kuwa kuanzia Usiku wa Ijumaa hadi jana imeendesha operesheni ya kijeshi iliyowezesha kudunguliwa kwa droni 10 za Ukraine kwenye anga yake.

Taarifa ya wizara hiyo ilisema ndege hizo zisizo na rubani zimedunguliwa na mifumo ya ulinzi wa anga.

Ndege tisa kati yake zilikuwa angani juu ya eneo la mkoa wa Belgorod, tano mkoa wa Voronezh, tatu juu ya Bahari Nyeusi na zilizobaki katika mkoa wa Kursk na Wilaya ya Krasnodar.

Hapo awali, Gavana wa Mkoa wa Voronezh, Alexey Gusev, aliandika kwamba hakukuwa na uharibifu au majeruhi katika eneo hilo kutokana na shambulio hilo.

**DW**



Wafanyakazi wa idara ya huduma za dharura nchini Israel wakiangalia eneo lililoshambuliwa na kombora ambalo jeshi lilisema lilirushwa kutoka Yemen na kutua Jaffa, kusini mwa Tel Aviv juzi. **PICHA: REUTERS**

## Wahouthi washambulia Israel yawajeruhi watu16

**TEL AVIV,** ISRAEL

WATU 16 wamejeruhiwa katika mji wa Tel Aviv nchini Israel baada ya shambulio la kombora lililorushwa na kundi la Wahouthi wa Yemen.

Shambulizi hilo la kombora ni la pili katika kipindi cha siku chache kufanywa na kundi hilo nchini Israel. Jeshi la Israel lilisema lilishindwa kulizuia kombora hilo, ambalo lilipiga katika mji huo mkuu wa kibiashara na kuwalazimu watu wengi kuzikimbia nyumba zao.

Waasi wa Houthi wa Yemen walidai kuhusika na shambulio hilo, wakisema walitumia kombora la masafa marefu wakiyalenga maeneo ya kijeshi ya Israel. Mara kadhaa waasi hao ambao wanaungwa mkono na Iran wamekuwa wakifanya mashambulizi ya makombora dhidi ya Israel wakitaka kuonesha uungaji mkono kwa Wapalestina katika vita vinavyoendelea Ukanda wa Gaza kwa zaidi ya mwaka mmoja.

Kufuatia shambulizi hilo, Israel imeyapiga maeneo kadhaa ndani ya Yemen ikiwemo bandari na vituo vya nishati vinavyosimamiwa na Wahouthi.

**DW**

# Marekani yaridhishwa utawala mpya Syria

**WASHINGTON,** MAREKANI

WANADIPLOMASIA wa Marekani wamesema wamekuwa na mazungumzo mazuri na kiongozi mpya wa Syria Ahmed Al-Sharaa kuhusiana na kipindi cha mpito cha kisiasa nchini humo.

Marekani iliwatuma wanadiplomasia wake wawili, Barbara Leaf, anayeshughulikia masuala ya Mashariki ya Kati na Roger Carstens ambaye ni mjumbe maalum wa masuala ya mateka kuzungumza na Al-Sharaa aliyeongoza kundi la waasi la Hayat Tahrir al-Sham, kuangusha utawala wa Rais Bashar Al-Assad wiki mbili zilizopita.

Leaf aliwaambia waandishi habari kuwa mazungumzo yao yalijikita juu ya umuhimu wa kuyadhibiti makundi ya kigaidi yasilete kitisho ndani na nje ya Syria.

Alisema kufuatia mazungumzo hayo ya kutia moyo, Marekani itaipatia Syria msaada wa dola milioni 10.

Ziara ya wanadiplomasia hao wa Marekani ilikuwa ya kwanza tangu kuangushwa utawala wa Assad.

Wakati huo huo, utawala mpya nchini Syria ulisema unataka kuchangia amani ya kikanda na kuongeza kuwa unapinga aina yoyote ya migawanyiko.

Taarifa hiyo ilitolewa juzi baada ya mkutano kati ya kiongozi mpya wa Syria, Ahmed al-Sharaa na ujumbe wa kidiplomasia wa Marekani.

Ulisema unataka kuthibitisha jukumu la Syria katika kukuza amani ya kikanda na kujenga ushirikiano wa kimkakati na nchi nyingine za eneo hilo.

Al-Sharaa, kiongozi wa kundi la Kiislamu la Hayat Tahrir al-Sham (HTS) lililonyakua mamlaka, alikuwa akilengwa na Marekani, lakini baada ya mawasiliano hayo rasmi na ya kwanza hapo jana, ilitangaza kuondoa zawadi ya kukamatwa kwake.

Ofisa mmoja wa Syria, aliliambia shirika la habari la AFP kwamba mkutano huo baina ya Al-Sharaa na ujumbe wa Marekani ulikuwa na matokeo chanya.

**DW**

HABARI/SAFU

# Wanakijiji waboreshewa matibabu

**Na Faustine Feliciane,**
SONGEA

KUKAMILIKA kwa ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya katika Kijiji cha Mdundwaro Kata ya Peramiho wilayani hapa Mkoa wa Ruvuma kumepunguza adha ya upatikanaji wa huduma za afya na vifo vya wananchi kwa kukosa matibabu.

Wakizungumza na waandishi wa habari kijijini hapo, wakazi wa maeneo hayo walisema uwepo wa watoa huduma katika kituo hicho kwa muda wote kumeboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa muda wote.

"Awali huduma katika kituo hiki ilikuwa inatolewa kwa masaa na kuna wakati watoa huduma wanakuwa hawapo hasa wakati wa mwishoni mwa wiki, wengi walikuwa wanakaa mbali, ilikuwa inatulazimu kusafiri kutoka kijijini kwenda Peramiho mjini au Songea, baadhi ya wagonjwa walikuwa wanapoteza maisha njiani,"

" Kwa sasa watoa huduma wapo kwa muda wote, hivyo hawana haja ya kusafiri kwenda mbali kufuata matibabu," alisema Agustino Luhwoga, Mkazi wa Kijiji cha Mdundwaro na Msimamizi wa kituo hicho.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Zawadi Mlapone, alisema mradi wa ujenzi wa nyumba hizo, kisima cha maji na matundu nane ya vyoo umeendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na kuboresha huduma za afya.

" Kwa sasa tunaomba Serikali au TASAF watusaidie gari la wagonjwa kuwasafirisha wale wanaotakiwa kwenda hospitali kubwa, Peramiho au Songea kwa ajili ya matibabu zaidi, " alisema Zawadi.

Hata hivyo, aliishukuru TASAF na Serikali kwa kuwajengea mradi huo.

Mratibu wa TASAF Manispaa ya Songea, Ahosana Ngunge, alisema mradi huo ulianza mwaka jana baada ya kuombwa na wananchi na kukamilika Machi mwaka huu.

"Mradi huu umeghalimu shilingi milioni 179 kujenga nyumba mbili za wafanyakazi wa kituo, matundu nane ya vyoo, kuchimba kisima na ujenzi wa kichomea taka," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Hassan Mtamba, aliishukuru TASAF kwa mradi huo na kuahidi kushirikiana na wananchi kutunza miundombinu na kutatua kero zilizobaki

# Majaliwa apongeza TANROADS kurejesha mawasiliano barabara kuu Singida - Manyara



**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa (pichani)ameipongeza Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa kurejesha mawasiliano ya barabara kuu ya Manyara - Singida ambayo iliathirika Desemba 3, 2023 wakati wa maafa ya maporomoko ya tope la Mlima Hanang.

Majaliwa alitoa pongezi hizo juzi wakati wa hafla ya uzinduzi wa nyumba 109 za waathirika wa maafa ya maporomoko ya tope zilizojengwa katika kitongoji cha Waret, kijiji cha Gidagamowd, Hanang mkoani Manyara.

Alisema serikali imefarijika kwa jitihada zilizofanywa na wizara kwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha miundombinu hiyo inarejea kama ilivyokuwa awali.

"Niwapongeze Wizara ya Ujenzi, nakuona Mheshimiwa (Godfrey) Kasekenya upo hapa. Mlifanya kazi nzuri na ya kupongezwa kuhakikisha barabara hii inarejea vizuri," alisema Majaliwa

Katika hafla hiyo Waziri Mkuu Majaliwa alizindua na kukabidhi hati za nyumba 109 ambazo 73 kati ya hizo zimejengwa na serikali kupitia Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT), 35 zimejengwa na Chama cha Msalaba Mwekundu na moja imejengwa na Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mbali na kukabidhi hati, pia alikabidhi majiko 109 ya nishati safi ya kupikia ambayo ni zawadi iliyotolewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa waathirika hao.

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Maradhi yote ugua, kuchacha usiombee



**Na Adam Fungamwango**

Simba Wanyika, katikati ya miaka ya 1970 hadi mwanzoni mwa 1980, walifyatua kibao walichokiita 'Kimada'. Ni wimbo unaomzungumzia jamaa mmoja anayelalamika baada ya kukimbiwa na mpenzi wake pamoja na marafiki zake.

WASWAHILI wanasema mvua ikikatika, mwamvuli siku zote unabaki kuwa mzigo.

Mara nyingi chunga sana kuwa karibu na kuwaamini kwa asilimia 100 watu wa karibu yako ambao wako na wewe kwa kukuhitaji na kukutumia.

Wale ambao wanaamini kuwa kila ulichobeba kinawafaa wao na si wewe. Siku zote wao wanaamini kuwa wewe hauna thamani kama wamemaliza kile ambacho kiliwaleta kwako.

Marafiki wa aina hii wapo wengi sana, lakini pia wapenzi wa aina hii wametapakaa kila kona.

Ugumu unabaki pale pale, mara nyingi huwezi kuwafahamu mpaka pale wameshakukamua tone ya senti ya mwisho. Na hapo ndipo utakapoona rangi zao halisi.

Walikuwa wanakwita kila aina ya jina zuri. Majina makubwa ya kukupamba na heshima juu kiasi cha kujisahau kuona unafanana na hivyo wanavyokusifia.

Siku utakapokuwa huna wadhifa, kazi, biashara zimefilisika au huna tena uwezo wa kuwapa wanachokitaka, wanabadilika kabisa na kuwa kama siyo wale.

Wanakubadilikia na kukubeza na kuonekana kama vile ulivyokuwa ukiwapa misaada ya kuwawezesha ulikuwa kama unajipendekeza tu. Hapo ndipo kinapokuwa kilio na kusaga meno.

Wako baadhi ya watu wenye maono, huwa angalau wanaanza kushtukia kabla hawajamaliza akiba walizobaki nazo. Haya yamewatokea watu wengi duniani, kiasi kwamba hata wanamuziki wengi wameshawahi kulibainisha hili.

Simba Wanyika, katikati ya miaka ya 1970 hadi mwanzoni mwa 1980, walifyatua kibao walichokiita 'Kimada'. Ni wimbo unaomzungumzia jamaa mmoja anayelalamika baada ya kukimbiwa na mpenzi wake pamoja na marafiki zake.

Jamaa anaomboleza mbele ya mpenzi wake akimwambia kuwa kumbe mapenzi yote aliyoyaonesha kwake ni kwa sababu tu ya madaraka aliyokuwa nayo. Kwa sasa ameshushwa cheo kazini, pesa zimemkimbia, mpenzi hamjali kutwa kucha kuzungumza na wale rafiki zake ambao walikuwa machawa wake, leo wamemchukulia hadi mpenzi wake. Wimbo huo ulioimbwa na Wilson Peter na George Peter ni huu hapa.

*"Kimada wangu ooo kimada hoo, umeanza madharau, kwa kuwa kazi sina pesa sina ooo. Nakumbuka tuliishi naye, ulikuta ni madaraka kijana. Penzi letu lilikuwa la furaha, wala sikudhania, tutatengana mimi na wewe.*

*Iyolele ooomama Iyolele ooomama. Madaraka sina, kimada wangu kanikimbia, anaranda na rafiki zangu mitaani.*

*Madaraka sina, kimada wangu kanikimbia, anaranda na rafiki zangu mitaani. Nisaidiwe na nani, rafiki zangu siwaoni eee, inabaki ni vicheko nipitapo ee."*

Ni mkasa wa kusikitisha, lakini haya ndiyo wanayotokea na kuwapata binadamu hapa duniani, kila kinachotokea ni somo kwa wengine.

Bendi ya Juwata Jazz, mwanzoni mwa miaka ya 1980, ilikuja na kibao walichokiita 'Faulata.'

Maudhui ni hayo hayo. Jamaa hana kazi, amechacha ile mbaya, mpenzi wake haona isiwe tabu, akamkimbia. Sasa jamaa analalamika, na kuthibitisha msemo usemao, mla nawe ni mfa nawe.

*"Ilikuwa siku ya Jumanne, asubuhi, nataka kwenda kazini, ndipo ulipotamka neno kuwa umechoka, kuishi na mimi. Kosa gani ewe Faulata, sikupata jibu jingine, ila sikutaki eee, sikutaki tu, kuchunguza kuchunguza kumbee, umempata mwingine awezaye kumiliki maisha yako kunishinda mimi.*

*"Ama kweli ee, maradhi yote ugua, lakini kuchacha usiombee.*

*Kumbukaa Faulata kila mpanda ngazi hushuka, usidanganyike, usidanganyike ooo hohoho we dada."*

*Nisikilize kwa makini haya ninayokwambia, kuibuka na kuchacha, Mola ndiye mpangaji wa yote. Ngazi hiyo wamepanda wengi na sasa wameshuka, nakuruhusu uende utaiona dunia eee. Umekuwa mzigo wa moto eee, haubebeki wala haushikiki, nakuruhusu uende utaiona dunia."*

Hii yote unatufunza kuishi na binadamu yoyote yule iwe mpenzi au rafiki kwa akili. Usimalize kila kitu. Tumia kile ambacho unaona hakiwezi kuathiri maisha yake ya baadaye hata kama utapata matatizo.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Nyuma ya Pazia-14

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

ALIPOFIKA alipanda daladala linaloelekea maeneo ya Tuangoma. Ilikuwa ni safari ndefu kidogo. Alifika Mikadi, Mjimwema, Kibada, Maliasili na alishuka kituo cha mbele. Hakukuwa na taa nyingi, kwani halikuwa eneo la makazi ya watu. Badala yake ni viwanda vikubwa vilivyojengwa kando ya barabara. Yeyote yule angeweza kuogopa, lakini kwa upande wa Eddy alipenda mazingira hayo. Aliona yatamrahisishia kazi na kuifanya kwa utulivu na uhakika na kiwango cha hali ya juu.

Alisogea hadi eneo ambalo aliambiwa kuwa ndiyo sehemu ya tukio. Alivuka barabara kwenda upande wa pili ambao hata kama kungekuwa na mtu au watu wanaomtazama wasingemtilia shaka.

Alionekana kama anapita eneo hilo bila wasiwasi wala kuonekana kama kuna kitu anahisi.

Alikwenda mbele kidogo, eneo ambalo barabara imeinuka kidogo, yaani mlima na kona kali.

Alipopita hapo alikata barabara isiyokuwa na lami iliyokuwa upande wa kushoto.

Akavuka tena barabara kuu ya kwenda Tuangoma, akaingia kwenye barabara nyingine ya vumbi.

Alienda nayo hadi alipohisi kuwa akikata kona upande mwingine na kushoto na kuambaa pori kwa pori anaweza kufika eneo lililotajwa na Macky kwa usahihi, bila kujulikana na mtu yeyote.

Alijua kabisa kuwa anakopita hawezi mtu yeyote ambaye hana shughuli maalum kupita pale.

Aliambaa kwenye pori hilo dogo taratibu kwa dakika kama tano hivi. Alihisi kuwa mbele kuna jengo.

Ni lile lile ambalo aliambiwa na Macky. Hapo aliinama chini na kuanza kutambaa ili kutomshtua yeyote ambaye atakuwa anakaribia hapo au kuwapo.

Aliangalia saa yake ilitimu saa mbili na nusu usiku. Ni muda ambao alijua watekaji watakuwa tayari wameshafika kama watakuwa hawajapata taarifa nyingine ya kuwatishia au kuwatonya.

Dakika kumi baadaye alianza kama kusikia minong'ono kutoka nyuma yake.

Hilo lilimfanya kuzidi kujificha kichakani ili asionekane.

Sio kama aliogopa, ila hakutaka yeyote amuone ili afahamu ni nini kinatendeka na ni nani.

Kazi aliyopewa licha ya kufanikisha mtoto kupatikana, lakini pia kufahamu kina nani wapo nyuma ya mpango huu na kwa nini awali siri zilikuwa zinavuja na nani alikuwa anavujisha.

Hilo lilimfanya asitake kabisa kuonekana yupo hapo, kwani kitendo cha watekaji kujua hilo litakuwa limeharibu mpango wote.

Na kweli, aliona watu wanne wakipita kando yake. "Tulimwambia aweke pale." Akasikika mmoja akinong'ona na walikwenda hadi eneo ambalo hata yeye aliambiwa na Macky kuwa ndipo pesa zilipotakiwa kuwekwa. Akatabasamu kwani alikuwa sahihi.

Baada ya kuhakikisha hilo, walionekana kuondoka hapo haraka. Wawili walikwenda upande wa kulia. Mmoja alikwenda upande wa kushoto, akavuka barabara kuu na kwenda kujibanza kwenye kibanda ambacho kinaonekana kama vile mchana kinafanyiwa biashara ya mama lishe hivi kwa watu wa viwandani.

Mmoja alirudi sehemu ambayo yeye yupo na alikuwa mbele yake kama hatua 12 hivi. Upande mwingine wa mbele kulikuwa na ukuta wa kiwanda, hivyo hakukuwa na mtu yeyote.

Mbu walikuwa wengi wakiifurahia damu yake ya moto kwa kuinyonya, lakini hakuthubutu kujipiga ili kuwaua, kwani kufanya hivyo kungewashtua wale watu.

Alikuwa na uhakika kuwa wale ndiyo watekaji na wamefuata pesa. Kwa mara ya kwanza ndiyo watekaji wamekuja kufuata pesa bila kushtuka kama wametegewa mtego kama ilivyokuwa huko nyuma.

Hii ilimthibitishia Eddy kuwa ni kweli kulikuwa na mtu au watu ndani ya waokozi wa mtoto aliyekuwa akivujisha siri.

Ni nani? Hicho ndicho alichokuwa akikisubiri. Kitu alichokuwa akijiuliza ni kwa nini safari hii ambayo polisi hawakushirikishwa watekaji wamefika eneo la tukio? Ni baadhi yao ndiyo walikuwa wanatoa siri kama wanawafuatilia? Mbona leo hawafuatiliwi wamekuja?

Wakati akiwaza hayo alikuwa anawatoa mbu kwenye mwili wake kwa staili ya kujifuta na si kujipiga.

Kwa mbali aliona kuna mtu anavuka barabara. Awali alidhani yule jamaa wa mwanzo aliyekwenda kukaa kwenye kibanda cha mama lishe. Haikuwa hivyo. Mtu aliyevuka alikuwa anamtambua.

Ni Macky. Alikuwa na mkoba wake mkononi. Anaukumbuka mkoba ule. Ni ule aliompa, ukiwa na pesa taslimu shilingi milioni 15 za Kitanzania kama walivyotaka watekaji.

Hata hivyo, Eddy anajua kuwa ndani hakukuwa na kiasi hicho cha pesa.

Kulikuwa na shilingi milioni tano tu. Pesa hizo halisi zilikuwa juu ya mkoba ule. Chini kulikuwa na maboksi ambayo yalikatwakatwa kitaalam na kuonekana kama pesa.

Ni yeye mwenyewe ndiye aliyekuwa amezipanga chini ya mkoba na juu yake kuweka pesa halisi shilingi milioni tano.

Baada ya kufanya kazi hiyo akiweka kitaalam, alimpelekea Macky nyumbani kwake.

Alifungua zipu na kumuonyesha juu tu. Eddy akamwambia Macky kuwa amezitoa kwa rafiki yake ambaye alimkopesha ili mtoto aachiwe, halafu baadaye watakuwa wakilipa taratibu akishirikiana na ndugu zake.

Ni mkopo kwa mwaka mmoja, kitu ambacho Macky alikubali. Macky alitembea kwa hatua za taratibu huku akiangalia huku na huku kuangalia kama kuna mtu yeyote anafuatilia nyendo zake. Baada ya kujidhihirisha kuwa hakuna, alisogea taratibu hadi eneo ambalo alitakiwa aweke mkoba wa pesa.

Alipofika alisita kidogo. Akasimama, lakini baadaye akapiga tena hatua mbili mbele.

Akatoa kamba ya mkoba zilizokuwa begani.

Akauweka chini. Akaingiza mkono wake mfukoni na kutoa simu yake ya mkononi.

Ni kama alikuwa anaangalia kama atapigiwa simu na watekaji.

Mara tatu nzima zoezi lilikufa, au liliahirishwa baada ya kupigiwa simu akiambiwa arejee na mkoba wake kwani waomegundua kuwa wanafuatiliwa na polisi ili kukamatwa. Safari hii hakukuwa na kitu kama hicho.

Ni kama Macky hakuamini. Akavuta hatua taratibu kurudi nyuma.

Alipofika barabarani akavuka na kuondoka eneo la tukio haraka kama alivyoamriwa na watekaji. Kitu kilichobaki kichwani kwake ni kesho kupata mtoto wake Macaire.

Watekaji walimwambia kama zoezi likifanikiwa atapigiwa simu saa nne kamili asubuhi na kuelekezwa ni wapi aende akamchukue mtoto wake, akiwa salama salimini.

Kitu ambacho Macky alikuwa na uhakika nao ni kwamba watekaji watakuja kuuchukua mzigo wao baadaye. Hakujua kuwa kuna watu watano kwenye eneo hilo walikuwa wakimwangalia kwa makini na wakifuatilia kila alichokuwa akikifanya.

Aliyekuwa makini zaidi kuliko wote ni Eddy. Alikuwa tayari ameshatoa bastola yake ambayo ina kiwambo cha kuzuia sauti.

Alikuwa tayari kwa lolote litakalotokea, au yeyote aliyetaka kumdhuru Macky.

Baada ya kuondoka, kilichobaki ni watekaji kusogelea mkoba na kuchukua pesa zao shilingi milioni 15 ambazo walizihitaji ili wamuachie mtoto Macaire.

**Itaendelea Jumapili**




**Kwa mbali aliona kuna mtu anavuka barabara. Awali alidhani yule jamaa wa mwanzo aliyekwenda kukaa kwenye kibanda cha mama lishe. Haikuwa hivyo. Mtu aliyevuka alikuwa anamtambua.**

HABARI BURUDANI



## MADEE AMSHUSHA ROMA MKATOLIKI

MWANAMUZIKI mkongwe, Madee, amesema hawezi kufikiria siku moja anaweza kufanya kazi na rapa Roma Mkatoliki, kwa sababu yeye levo yake ni kuimba na Dogo Janja.

Akizungumza hivi karibuni, Madee amesema kutokana na ukongwe wake ni jambo lisilowezekana kufanya kolabo na wanamuziki wanaoinukia sasa kwani haitawezekana.

Amesema hata katika mazingira ya kazi hawako karibu sana, kiasi kila mmoja anajua wimbo wake mpya kupitia majukwaa ya muziki na sio kutumiana kama ilivyokuwa kwa wengine.

# NDOA YA MARIOO, PAULA YANUKIA

MWANAMUZIKI maarufu wa Bongo Fleva, Marioo, amesisitiza kwamba watu wajiandae kushuhudia ndoa yake na Paula Kajala.

Akizungumza na EATV, Marioo amesema kwamba kilichokuwa wanasubiri ni kuona mwenendo mzuri wa mtoto wao, jambo ambalo wanamshukuru Mungu anaendelea kukua bila matatizo yoyote.

Amesema, tayari Paula amekubali kubadili dini kinachoendelea ni kuweka vizuri mazingira ya namna ya harusi hiyo itakavyokuwa.

"Ndoa ipo kwa neema ya Mungu, kwa jinsi mwenendo unavyokwenda kwa mtoto wetu kila kitu kinaashiria kitakwenda vizuri. Kuhusu dini nafikiri yeye atakuja kwangu kwa sababu yeye kuja huku ni karibu zaidi," amesema Marioo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MAN YAMTAKA MUANI
MANCHESTER United ina nia ya kumsajili fowadi wa Ufaransa, Randal Kolo Muani mwenye umri wa miaka 26, kutoka PSG na huenda likawa chaguo la mkopo ambalo lina kifungu cha kumnunua jumla Januari. **(L'Equipe)**

### CHRISTENSEN AWANIWA
KLABU ya Newcastle United inalenga kumnunua mlinzi wa Barcelona, Andreas Christensen mwenye umri wa miaka 28, na kumuuza mchezaji huyo wa Kimataifa wa Denmark kunaweza kuruhusu klabu hiyo ya LaLiga kumsajili mshambuliaji wa Hispania, Dani Olmo mwenye umri wa miaka 26. **(Fichajes)**

### TRIPPIER KUPIGWA BEI
NEWCASTLE United pia inapanga kumuuza beki wa kushoto wa England, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 34, na kiungo mshambuliaji wa Paraguay, Miguel Almiron mwenye miaka 30, ili kusaidia msimamo wao linapokuja suala la sheria za faida na uendelevu. (**Football Insider**)

### CHUKWUEMEKA KUONDOKA
CHELSEA iko tayari kuwaruhusu wachezaji wa kati wa England, Kiernan Dewsbury-Hall mwenye umri wa miaka 26 na Carney Chukwuemeka (21), kuondoka kwa mkopo katika klabu hiyo Januari mwakani. (**Mirror**)

### HALL KUREJESHWA LEICESTER
LEICESTER City inapanga kumrejesha klabuni hapo, Kiernan Dewsbury-Hall, baada ya kumuuza kwa Chelsea kipindi cha majira ya joto. (**Football Insider)**

### POTTER ALIIKATAA WOLVES
KOCHA wa zamani wa Brighton na Chelsea, Graham Potter, alikataa nia ya Wolves mwezi uliopita huku klabu hiyo ya Midlands ikitafuta chaguo kuchukua nafasi ya Gary O'Neil, ambaye kwa sasa ametimuliwa. **(Guardian)**

### JACKSON NA ASTON VILLA
MSHAMBULIAJI wa Senegal, Nicolas Jackson nusura ajiunge na Aston Villa na Bournemouth kutoka Villarreal Januari 2023 kabla ya kwenda Chelsea. (**90min)**

### PULISIC MKATABA MPYA
KLABU ya AC Milan ya Italia inakaribia kumpata mshambuliaji wa Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 26 kwa mkataba mpya. (**Fabrizio Romano)**

### REIJNDERS, MAIGNAN NAO
AC Milan pia wanatazamia kuongeza mkataba wa kiungo wa kati wa Uholanzi, Tijjani Reijnders na kipa wa Ufaransa, Mike Maignan kwa masharti mapya na yaliyoboreshwa. (**Calciomercato**)

### MILLER SASA ALENGWA
KIUNGO wa kati wa Motherwell na Scotland, Lennon Miller mwenye umri wa miaka 18, pia analengwa na Liverpool na anaweza kupatikana kwa pauni milioni nane. (**Caught Offside**)

### BETO KUREJEA ITALIA
BETO wa Everton mwenye umri wa miaka 26, anaweza kurejea Italia Januari, huku Torino ikimtaka mshambuliaji huyo wa Guinea-Bissau. (**Tuttomercartoweb**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DIAS AONGEZA MAJANGA MAPYA MANCHESTER CITY

**MANCHESTER,** England

●●● Atakuwa nje kwa muda mrefu, alipata tatizo la misuli baada ya dakika 75 dhidi ya United, alihisi kitu...

PEP Guardiola amethibitisha imani yake katika mabadiliko ya Manchester City licha ya kubainisha pigo jipya la jeraha, ambapo mlinzi Ruben Dias atakuwa nje ya dimba kwa mwezi mmoja.

**Kipigo cha Jumapili iliyopita cha mabao 2-1 kutoka kwa Manchester United kilizidisha mzozo wa Man City, huku mabingwa hao wa Ligi Kuu England wakipoteza michezo nane kati ya 11 iliyopita na kukaa pointi tisa nyuma ya vinara Liverpool.**

Guardiola alidai kuwa "sifai vya kutosha" baada ya mechi hiyo kwenye Uwanja wa Etihad, lakini anabakia na uhakika wa kuimarika.

"Tulikaribia kushinda na tukapoteza mchezo," alisema Guardiola kuhusu mchezo wa Manchester dabi. "Sikuwa na furaha na ilibidi niwe mkweli kwangu.

"Unaanguka mara sita, lazima usimame. Mimi ni mtu wa kawaida mwenye hisia kama sisi sote.

"Hali inapoenda vizuri tunakuwa bora zaidi na wakati haiendi vizuri kitaaluma tunazingatia zaidi kile tunachopaswa kufanya.

"Mapema au baadaye, tutaigeuza. Sijui lini."

Lakini City wanaweza kukabiliwa na tatizo katika safu ya ulinzi, licha ya Manuel Akanji na John Stones kurejea mazoezini, huku Dias akipata jeraha la misuli dhidi ya United.

"Yeye (Dias) yuko nje kwa muda mrefu. Wiki tatu au nne. Tatizo la misuli. Baada ya dakika 75 dhidi ya United alihisi kitu, lakini ana nguvu sana hivyo alibaki uwanjani."

# JAMES AREJEA MAZOEZINI CHELSEA



**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Enzo Maresca, amethibitisha kuwa Reece James amerejea kwenye mazoezi baada ya jeraha lake la msuli wa paja, lakini Benoit Badiashile na Wesley Fofana watakuwa nje hadi mwakani.

James amefanikiwa kucheza mechi nne pekee katika mashindano yote msimu huu, akiwa ameanza msimu na tatizo la misuli ya paja kabla ya kupata tatizo jipya mwishoni mwa Novemba ambalo limemfanya kuwa nje ya uwanja tangu wakati huo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, hivi majuzi alionekana akikimbia tena na Maresca alithibitisha katika mkutano wake na waandishi wa habari kwamba ataongeza ahueni yake kwa kurejea kwenye mazoezi.

"Reece hatimaye ameanza mazoezi, kwa hiyo polepole atarejea," alisema kocha huyo raia wa Italia.

"Mpango wake ni kuwa na timu kwa sehemu ya kikao na kutoka hapo kujaribu kumjengea hali sahihi na hatimaye anaweza kurejea nasi."

Kurejea kwa James kwenye mechi ya ushindani bado kunaonekana wiki kadhaa zimesalia na ndivyo hali ilivyo kwa mabeki Badiashile na Fofana.

"Wote wawili bado wako nje na wote watakuwa nje kwa muda mrefu," alisema Maresca kabla ya kuthibitisha kwamba hakuna mchezaji atakayerejea kabla ya Januari.

Kiungo Romeo Lavia atakabiliwa na kipimo cha utimamu wa mwili akiwa amechelewa kabla ya Maresca kufanya uamuzi wa mwisho kuhusu kupatikana kwake, lakini Chelsea hawana matatizo mengine ya majeruhi kwa sasa.

# Mount nje ya dimba muda mrefu




**MANCHESTER,** England

RUBEN Amorim amefichua kuwa Mason Mount yuko mbioni kukaa nje kwa muda mrefu baada ya jeraha lake la hivi karibuni katika ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Manchester City.

Kiungo huyo alilazimika kutolewa nje baada ya dakika 14 kwenye Uwanja wa Etihad ikiwa ni mara yake ya nne tu kuanza kwenye Ligi Kuu England msimu huu.

Mount alionana na mtaalamu Jumatano ili kubaini ukubwa wa jeraha lake.

Alipoulizwa Mount atakuwa nje kwa muda gani, Amorim alijibu: "Wiki kadhaa. Sijui tarehe kamili, lakini utakuwa muda mrefu na ndivyo hivyo. Hiyo ni sehemu ya soka."

Mount amekuwa akipambana na majeraha kwa muda wote aliokaa Old Trafford. Kipindi cha miezi 18 katika klabu hiyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, amemaliza dakika 90 mara moja na hajawahi kucheza Ligi Kuu.

"Ninachoweza kufanya ni kumsaidia Mase kumfundisha jinsi ya kucheza mchezo wetu," alisema Amorim.

"Anapopata nafuu, jaribu kutumia muda huo kwa mambo tofauti, mbaya zaidi ni kwamba hatuna muda wa kufanya mazoezi kama tunavyopaswa kufanya baada ya majeraha mengi.

"Ni ngumu sana kutengeneza upya mchezo kabla hawajafika kwenye mchezo, tukiwa na Mason tutamsaidia, ni ngumu sana kwa mchezaji kukaa nje kwa muda mrefu, anajaribu sana, wakijaribu sana tutamsaidia."

# Dele Alli athibitisha kuondoka Everton

**LONDON,** England

DELE Alli amethibitisha hatma yake ya baadaye iko mbali na Everton licha ya kuendelea na mazoezi katika klabu hiyo tangu mkataba wake ulipomalizika majira ya joto.

Alli alijiunga na Everton akitokea Tottenham Hotspur Januari 2022, lakini alianza mara moja tu kwenye Ligi Kuu England kwa klabu hiyo ya Merseyside, pamoja na mechi 12 akitokea benchi.

Hajacheza soka la ushindani tangu Februari 2023, alipokuwa kwa mkopo katika Klabu ya Besiktas ya Uturuki, na mwaka jana alikaa kwa muda wa wiki sita katika kituo cha kurekebisha tabia nchini Marekani kwa ajili ya uraibu na afya ya akili.

Amekuwa akijaribu kupata nafuu kutokana na masuala kadhaa ya utimamu wa mwili.

Hata hivyo, kiungo huyo sasa anaonekana kuanza safari mpya mbali na Merseyside na ametoa shukrani zake kwa usaidizi ambao Everton wamemuonesha wakati akiwa klabuni hapo.

Katika ujumbe wake kupitia Instagram, Alli alisema: "Mwaka 2025 unaweza kuniweka kwenye njia mpya yenye fursa za kusisimua. Kabla ya hayo kutokea, ni muhimu sana kwangu kuweka wazi jinsi ninavyowashukuru mashabiki, wafanyakazi na wachezaji wote Everton FC kwa sapoti waliyonipa.

"Imekuwa safari ngumu sana kujaribu kuweka vitu vyote sawa ili kurejesha utimamu wa mechi na nawashukuru wafanyakazi wa Everton vya kutosha kwa kazi kubwa waliyoweka katika mchakato huu," aliongeza.

"Kwa bahati mbaya, mambo hayajafanyika kama tulivyotarajia sote, na nadhani ni wakati muafaka kwangu kufungua ukurasa mpya. Ninataka kuwatakia kila la heri katika klabu hii."

HABARI MICHEZO

# RAMOVIC: NI USHINDI TU LEO

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesema wanachohitaji kwenye mchezo wa leo ni pointi tatu tu na hakuna kingine, kwani ndicho kinachosubiriwa na wanachama na mashabiki wa timu yake ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kuelekea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Yanga leo inashuka tena kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, kucheza dhidi ya Maafande wa Prisons, timu ambayo haijashinda mchezo wowote kati ya minne iliyocheza mfululizo.

Kocha huyo raia wa Ujerumani, amesema wala hawatoidharau Prisons kutokana na matokeo yake mabaya kwenye Ligi Kuu, au nafasi iliyonayo kwa sasa, badala yake wataingia uwanjani wakiwa na malengo yao ya kupata ushindi ili kujiwekea mazingira mazuri ya kutwaa ubingwa ambao anasema vita inaonekana kuwa kubwa kileleni.

"Maandalizi tayari, itakuwa mechi ngumu, tunacheza na timu inayokabia chini na kushambulia kwa kushtukiza, inatakiwa tuwe makini ili kushinda mechi hii, tutafanya kila linalowezekana kushinda mechi hii kwani tunahitaji pointi tatu.

"Hatuwezi kuidharau Prisons kwa sababu ya matokeo yake mabaya, tunatakiwa kuiheshimu kila timu, mpira wa miguu ni mchezo wa ajabu sana ambao mwisho wa siku unaweza kuumiza moyo wako kwa sababu ya dharau," alisema kocha huyo.



Yanga itacheza mchezo wa 13 leo, ikiwa na pointi 30, na kama ikishinda itafikisha pointi 33 ambazo kwa sasa inazo Azam FC ambayo imeshamaliza mechi zake za mzunguko wa kwanza.

Kabla ya mchezo wa leo, Yanga imecheza michezo 12, ikishinda 10, ikipoteza miwili, haijatoka sare hata moja, ina mabao 19, ikiruhusu sita nyavuni kwake.

Kwa upande wa Prisons, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Shaaban Mtupa, alisema alikuwa na kazi kubwa ya kuwarudisha kwenye morali wachezaji wake ambao walionekana kama wamekata tamaa kutokana na matokeo mabaya ya siku za hivi karibuni.

Hata hivyo, alisema kazi yake imezaa matunda kwani wachezaji wa Prisons sasa wamemka na wako tayari kwa mchezo huo.

"Kazi ya kwanza niliyoifanya kubwa ni kurudisha ari ya wachezaji ambao inaonekana kabisa ilikuwa chini, kingine ni kuwafanya wajiamini, hivi vipindi vya mpito hata sisi wakati tunacheza mpira tumevipitia.

"Kwa sasa naona wameamka na wapo tayari kwa mchezo wa kesho. Ni muhimu sana kwetu kwa sababu hatujapata matokeo mazuri mechi kadhaa nyuma, lakini sasa tunahangaika kupata matokeo ya ushindi," alisema straika wa zamani wa timu hiyo.

Hata hivyo alikiri haitokuwa mechi rahisi kutokana na ubora wa timu ambayo wanakwenda kukutana nayo.

" Tunakwenda kucheza na Yanga ambayo ni timu nzuri sana na wachezaji wanaoweza kuamua matokeo muda wowote, lakini na sisi tumeyafanyia kazi, tunataka kutumia udhaifu waliokuwa nao kuwaadhibu ili kupata ushindi," alisema.

Kwa sasa Prisons inakamata nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 11 kwa michezo 14 iliyocheza.

Mara ya mwisho kupata ushindi ilikuwa Novemba 3, mwaka huu, Uwanja wa Sokoine Mbeya, iliposhinda bao 1-0 dhidi ya KenGold, baada ya hapo ilichapwa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania, mabao 2-1 dhidi ya Coastal Union, suluhu dhidi ya Kagera Sugar na kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Singida Black Stars.

## Tanzania yapania ubingwa wa CHAN

INATOKA UK. 24

Naye Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema anaahidi hawatamwangusha Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha 'maono' ya Watanzania yanatekelezeka.

Karia alisema uongozi wake wa miaka saba umekuwa na mafanikio, lakini mwaka 2024, umekuwa na mafanikio zaidi.

Alisema Taifa Stars imefuzu kushiriki Fainali za AFCON, Twiga Stars nayo imekata tiketi ya kushiriki WAFCON sambana na Timu ya Vijana ya umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes).

Alisema pia yosso wavulana wa U-15 pia wametwaa ubingwa wa CECAFA huku Serengeti Boys iliyotinga hatua ya nusu fainali imekaribia kufuzu tiketi ya AFCON U-17.

"Haikuwa rahisi kufikia mafanikio haya, mafanikio yote yametokana na mpango mkakati tuliokuwa nayo, matunda ya kuwekeza katika vijana yanalipa, tumewekeza zaidi katika ligi za vijana na wanawake," Karia alisema.

Aliwataka wadau kuacha kueneza propaganda kuhusiana na maandalizi kuelekea fainali za CHAN na kufafanua nchi mojawapo ikishindwa kufikia vigezo, basi Afrika Mashariki itakuwa imepoteza nafasi ya kuwa wenyeji wa fainali hizo za CHAN na AFCON 2027.

Alisema pia kwa kushirikiana na wadhamini Azam Media na serikali, watahakikisha VAR inaanza kutumika kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**KARIA MGOMBEA PEKEE**

Wajumbe wa mkutano Mkuu wa TFF jana waliadhimia kumpitisha Karia kuwa mgombea pekee wa nafasi ya rais wa shirikisho hilo linalotarajia kufanya uchaguzi wake mkuu mwakani.

Uamuzi huo ulifikiwa baada ya Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu, kuwasilisha hoja hiyo kwa wajumbe wa mkutano huo kwa kusema Karia anastahili kuendelea kuiongoza TFF.

"Karia amefanya kila kitu, tumpeni maua yake, huyo anayekuja atafanya nini, naomba tuadhimie kumpitisha kuwa rais kwa kipindi kingine, mwakani uchaguzi uwe wa wajumbe wa Kamati ya Utendaji," Mangungu alisema.

Hersi Said, Rais wa Yanga, naye aliungana na Mangungu na kuipongeza Kamati ya Utendaji ya TFF kwa kazi nzuri wanayofanya.

Hersi alisema Karia anastahili kuendelea kuiongoza TFF kwa sababu ameweza kuipa mafanikio ambayo huko nyuma ilikuwa ni kama haiwezekani.

Wakati huo huo, mkutano huo umepitisha bajeti ya Sh.bilioni 56.3 ambayo inatarajiwa kukusanywa huku matumizi yakiwa ni Sh. bilioni 56.1 yakitarajiwa kutumika katika mwaka ujao wa fedha.

## *Mpanzu moto mkali Simba ikikaa kileleni*

INATOKA UK. 24

zia kazi kubwa iliyofanywa na Chasambi kwa mara nyingine.

Straika huyo anatimiza bao la nne kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, ukiwa ni msimu wake wa kwanza akiwa amesajiliwa kutoka Asante Kotoko ya Ghana.

Dakika za majeruhi, Cleophace Mkandala alipiga shuti kali la mbali ambalo lilikwenda moja kwa moja hadi wavuni na kumuacha kipa Moussa Camara akiruka bila mafanikio, likiwa ni bao la pili la Kagera Sugar katika mchezo huo.

Simba ilianza mpira kwa kasi na sekunde ya 32 tu tayari walikuwa wamefika kwenye lango la wenyeji wao kwa kugongeana, mpira ulimfikia, Jean Ahoua aliyepiga shuti la mbali mpira ulionekana kama unataka kutinga wavuni, lakini ukatoka juu kidogo ya lango.

Kagera Sugar ilijibu shambulio hilo dakika ya nne, pale walipowanyang'anya mpira wachezaji wa Simba waliokuwa wameanzia nyuma, pasi ya mwisho ilifika kwa Geofrey Manyasi ambaye shuti lake lilitoka pembeni kidogo ya lango.

Dakika ya sita, nusura Debora Fernandes aipatia Simba bao, baada ya shuti lake lililoonekana kwenda wavuni kumgonga David Luhende na kurejea uwanjani kabla ya kuokolewa.

Shambulizi hilo lilifanywa na Mpanzu aliyekuwa akicheza mechi ya kwanza akiwa na timu hiyo, akishirikiana na Kapombe.

Kipigo hicho kinaiacha Kagera Sugar katika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 11, na ikiwa imemaliza michezo yake ya mzunguko wa kwanza.

## Morrison ataka mil. 10/- kutua KenGold, Bwalya Pamba Jiji

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha dogo la usajili likiwa wazi tangu Desemba 15, mwaka huu, na klabu mbalimbali zikihaha huku na kule kusaka wachezaji kwa ajili ya kuviongozea nguvu vikosi vyao kuelekea hatua ya mzunguko wa pili Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa kuwa winga mtukutu wa zamani wa Klabu za Simba na Yanga, Benard Morrison, huenda akatua KenGold kama watatekeleza kile ambacho anakihitaji.

Aidha, Pamba Jiji nayo ipo kwenye mazungumzo na Klabu ya Napsa Stars ya Zambia kumtwaa Larry Bwalya.

Habari kutoka ndani ya Klabu ya KenGold, zinasema kuwa wamezungumza na Morrison na amekubali kujiunga na timu hiyo kama watampa mshahara wa Sh. milioni 10 kwa mwezi.

"Hivi tuko kwenye majadiliano kama tunaweza kufanya hivyo. Tutaangalia vitu vingi, bajeti na mambo mengine ya kiutawala kwani wachezaji wengi wanaoichezea timu hii mshahara wao haufiki hata nusu ya hiyo pesa, isiwe tukamchukua halafu ilete matatizo kwa wachezaji wengine. Pamoja na yote ni mchezaji mzuri, kama atakuwa kwenye kiwango kile ambacho tunakijua, basi KenGold itatisha. Tusubiri tuone hali itakuwaje, kama ikienda sawa tutamtangaza, lakini kama mkiona kimya ujue imeshindikana," alisema mtoa taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo.

Morrions raia wa Ghana, aliyechezea Yanga kwa misimu miwili tofauti na Simba, kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake na FAR Rabat ya Morocco, ambayo alishindwa kuitumikia kwa muda mrefu kutokana na kuwa majeruhi.

Wakati hayo yakiendelea, Klabu ya Pamba Jiji imetajwa kuwa kwenye mazungumzo ya kumsajili kwa mkopo wa miezi sita, kiungo mshambuliaji wa zamani wa Simba, Bwalya.

Vyanzo zinasema kuwa mkataba huo una kipengele cha kumsajili mchezaji huyo jumla mwishoni mwa msimu iwapo itavutiwa na uwezo wake.

Kama akijiunga na klabu hiyo, hatokuwa mgeni kwenye Ligi Kuu, kwani aliichezea Simba, akijiunga nayo 2020 akitokea Power Dynamos ya Zambia, hadi 2022 alipotimkia Amazulu FC ya Afrika Kusini na mwaka mmoja baadaye, Shekhukhune pia ya huko, kabla ya kujiunga na Napsa Stars ya nchini kwao Zambia mwanzoni mwa msimu huu.

# Michezo

Jumapili Desemba 22, 2024

Nipashe




Ramovic: Ni ushindi tu leo

UK. 23

# Mpanzu moto mkali Simba ikikaa kileleni

## Kagera Sugar yala mkono, Mukwala, Ahoua, Chasambi wakionesha ubora wao wa...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO matano yaliyofungwa na Shomari Kapombe, Jean Ahoua, Fabrice Ngoma na Steven Mukwala aliyepachika mawili, jana yaliirejesha kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kupata ushindi wa 5-2 dhidi ya Kagera Sugar katika mchezo mkali wa aina yake uliochezwa Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

Simba imekuwa ikihangaika kupata ushindi kwenye uwanja huo kwa misimu mitatu sasa ambapo ilikuwa ikiambulia sare na kichapo.

Ushindi huo umeifanya kuongoza ligi, ikifikisha jumla ya pointi 34, mabao 29 ya kufunga, kuruhusu matano nyavuni mwake hadi sasa ikiwa imecheza mechi 13.

Unakuwa ni ushindi mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, kwani hakuna timu yoyote iliyowahi kupata idadi hiyo ya mabao kabla.

Mechi hiyo pia imeweka rekodi ya kuwa na mabao mengi zaidi kwenye ligi mpaka sasa, kutokana na kuzaliwa mabao saba kwenye mchezo mmoja.

Moja ya tukio ambalo wanachama na mashabiki wa Simba walifurahia ni kumuona kiungo mshambuliaji wao mpya, Elie Mpanzu, akiichezea timu hiyo kwa mara ya kwanza, kama walivyotarajia alikuwa kwenye kiwango kikubwa ambacho kilichangia ushindi huo.

Shomari Kapombe ndiye alianza kufungua kitabu cha mabao dakika ya 12 ya mchezo, alipounganisha krosi iliyopigwa na Mohamed Hussein, 'Tshabalala'.

Mpira ulianzia kwa Ahoua, ambaye aliupeleka pembeni upande wa kushoto, beki huyo akiwa amepanda mbele alimimina krosi ambayo Steven Mukwala aliruka juu na kuukosa mpira, lakini Kapombe alikuwa kwenye eneo zuri akaukwamisha wavuni.

Ni bao la pili kwa beki huyo wa kulia wa Simba msimu huu, huku Tshabalala naye akifikisha 'asisti' ya tatu.

Alikuwa ni Ahoua, aliyeiandikia Simba bao la pili kwa mkwaju wa faulo dakika moja kabla ya mapumziko, baada ya yeye mwenyewe kuchezewa madhambi na Abdallah Mfuko, nje kidogo ya eneo la hatari.

Kiungo mshambuliaji huyo raia wa Ivory Coast, aliupitisha mpira juu ya vichwa vya wachezaji na kugonga mwamba wa juu, ukadundia ndani na kurudi uwanjani, huku mwamuzi Tatu Malongo akiita kati baada ya kupata ishara kwa msaidizi wake kuwa ulikuwa umevuka mstari.

Linakuwa bao la sita kwa mchezaji huyo msimu huu, akiwa ndiye anaongoza kwa ufungaji mabao katika kikosi hicho.

Dakika ya 40, kiungo mshambuliaji wa Simba, Awesu Awesu alilazimika kutoka nje kutokana na kuumia na nafasi yake ilichukuliwa na Ladack Chasambi, ambaye alitoa 'asisti' tatu, mbili kwa straika wa Uganda, Mukwala na moja kwa Fabrice Ngoma.

Kiungo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Ngoma, aliipatia Simba bao la tatu dakika ya 53 kwa kichwa, akiunganisha mpira wa kona uliopigwa na Chasambi.

Kona hiyo ilitokana na Debora Fernandes kupiga shuti kali karibu na eneo la hatari ambalo lilimbabatiza Mohamed Mussa na kuwa kona.

Mukwala alipachika bao la nne, dakika ya 66 baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Chasambi, kuwatoka mabeki wa Kagera Sugar na kumwekea mfungaji kwenye nafasi nzuri, ambapo alitisha kama anapiga na mguu wa kulia, hali iliyosababisha Mfuko na kipa wake Ramadhani Chalamanda kupoteana na kumpa nafasi mfungaji kumalizia kwa mguu wa kushoto.

Ilionekana kama Simba na Kocha Fadlu Davids na wachezaji wake waliridhika na mabao hayo, wakafanya mabadiliko ambayo yaliyonekana kuwaathiri na kuruhusu mabao mawili dakika za mwishoni mwa mchezo.

Walioingia ni Joshua Mutale, Kelvin Kijili, Yusuph Kagoma, badala ya Mpanzu, Ngoma na Mavambo.

Mabadiliko hayo yalionekana kuwafanya wenyeji kupata uhai na kulishambulia kama nyuki lango la wapinzani wao.

Alikuwa ni Datius Peter aliyeipatia Kagera Sugar bao la kwanza dakika ya 79, akionekana kusahaliwa na mabeki wa Simba, akaingia ndani ya eneo la hatari na kuukwamisha wavuni.

Mukwala alifunga bao la tano dakika tano kabla ya mchezo kumalizika, akimali-

INAENDELEA UK 23



Mpanzu

# Tanzania yapania ubingwa wa CHAN

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SERIKALI imesema itahakikisha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inatwaa ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), lakini pia kuvuka hatua ya makundi kwenye Fainali za AFCON zitakazofanyika mwakani.

Tanzania, Kenya na Uganda ndio wenyeji wa Fainali za CHAN zitakazofanyika Februari mwakani.

Akizungumza katika ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa mwaka wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA', alisema serikali imeandaa mazingira bora ya kuiandaa Stars ili ivunje rekodi katika fainali hizo.

Mwana FA alisema serikali imeahidi kutimiza mahitaji yote yanayotakiwa kukamilisha kama nchi mwenyeji na itafanya hivyo mapema kama ilivyotarajiwa.

Alisema wanataka kuona Tanzania inajiweka katika nafasi nzuri kama mwenyeji na timu inayoshiriki kuonesha ushindani.

"Tunataka kuvunja rekodi, hatutaishia raundi ya kwanza, mimi napenda sifa na sifa hiyo ninaitaka, tumeweka malengo ya kukata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa mwaka 2030," alisema Mwana FA.

Aliwapongeza wajumbe wa mkutano Mkuu wa TFF kwa kuendelea kufanya kazi nzuri mikoani na hiyo imesaidia kuifanya Ligi Kuu ya Tanzania Bara kuwa moja ya ligi za daraja la juu Afrika.

"Kujadili maendeleo ni jambo la msingi, mkutano huu ndio unatumika kujadili, kuwasilishwa na kutelekezwa mipango ya maendeleo, mnafanya kazi kubwa sana, ninawapongeza," alisema waziri huyo.

INAENDELEA UK 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042